

ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA

 Asante, Ndugu. Mungu akubariki. Hilo ni zuri sana.

² Yeyote ambaye hangeweza kuhubiri nyuma ya hilo hangeitwa mhubiri, sivyo? Ajabu, inapendeza, imefanywa vyema. Hakika nashukuru kwa ajili ya hilo katika ndugu yangu mpendwa. Nilikuwa tu nikiuliza juu yake, jinsi alikuwa karibu kwa ajili ya huo mkutano mwingine, lakini nadhani anatoka, sikulipata vizuri, kutoka mkoa mwingine ama kitu fulani. Lakini hiyo ni nzuri sana. Nashukuru sana kwamba Mungu amempa huyu ndugu kipaji hiki kizuri sana cha kuimba sifa Zake. Mnajua, yana—yote yanaenda kufanya Injili. Nilikuwa nikihubiri hivi majuzi, Mikoani kule, juu ya *Njia Nne Za Kumwona Mungu*. Mwajua, na kuna njia elfu moja za kumwona Mungu kama tutaangalia tu kote. Yeye ni—Yeye yuko kila mahali.

³ Sasa, tunasikitika kwamba tuliwaweka sana jana usiku, wakati mlikuwa na joto sana humu ndani. Baadhi ya marafiki walio pamoja nami walisema, “Whiu!” Walikuwa wakijipepea tu. Kwa hiyo mimi...Kisha mtu fulani akasema, “Hiyo haiwasumbui Wahindi hata hivyo,” kasema, “wanakesha pale pale usiku kucha, wakishuhudia usiku kucha.” Kwa hiyo—kwa hiyo ninashukuru. Labda ninapoondoka, unasimama tu na kuanza kushuhudia, ukisimulia yale Bwana aliyokutendea.

⁴ Ni wangapi wenu husikia habari za Tommy Osborn? Yeye ni rafiki yangu wa thamani sana, naye huenda kwenye nchi ya kale sana, ng'ambo ya bahari, mmishenari. Naye alisema... Wakati mmoja nilikuwa ninaenda... Nilikuwa nikienda zangu Afrika Kusini, naye akaja kwenye huo mkutano. Ndipo—ndipo nilipotoka jukwaani huko—huko kwenye Jiji la New York, mahali ambapo wanashindana hiyo miereka yote, uwanja mkubwa wa michezo kule, napo mahali hapo palikuwa pamejaa sana na kusongamana, nami nilikuwa nikipita jukwaani, ndipo Tommy akaja hapo moja kwa moja na kunishika kiunoni na kuanza kunikumbatia. Nami nikasema, “Tommy, unafanya nini hapa juu?”

⁵ Kasema, “Kukuaga tu kwaheri na kuomba baraka za Mungu juu yako wakati ukienda ng'ambo.” Yeye ni mmoja wa waongofu wangu kwa Kristo, katika huduma ya uponyaji. Naye akasema...

Nami nikasema, “Nadhani umechoka sana, Tommy. Umekuwa ukihubiri sana.”

⁶ Kasema, “La,” kasema, “Sina upambanuzi wowote na inanibidi kuchoka sana.” Kasema, “Unajua ninachofanya? Ninasimama tu pale kwa dakika kumi na tano na kumfunga ibilisi katika fundo kwa Neno,” kasema, “hawezi kujitoa humo. Kisha ninawafanya waombeane, na halafu ninajitafutia kiti na kuketi, nawasikiliza wakishuhudia mpaka mapambazuko,” akasema. Kasema, “Mmoja atasimama na kushuhudia na kusema yale Mungu aliyomtendea, na akasema hilo humfanya mwingine kuamini, naye anasimama na kushuhudia, na huku akishuhudia mwingine anasimama.” Kisha akasema, “Mimi naketi tu hapo, na kupiga makofi yangu, na kuwa na wakati mzuri.” Loo, jamani.

⁷ Inapendeza sana kuona jinsi Mungu alivyo na huduma Zake mbalimbali, mnaona, jinsi anavyozifanyiza kazi. Ndugu huyu mpendwa, hapa, anayeimba, hiyo ni huduma ya nyimbo. Na wengine wana huduma. Mnaona, Mungu ameweka Kanisani karama zilizokusudiwa tangu zamani, moja ya hizo ni, ya kwanza ni mitume, manabii, walimu, wachungaji, na wainjilisti.

⁸ Sasa, mitume hasa ni wale tungewaita leo, tunawapa jina jipya, mmishenari. Mmishenari ni mtume. Sasa, neno *mmishenari* linamaanisha “aliyetumwa,” na *mtume* maana yake ni “aliyetumwa,” kitu kile kile. Lakini jinsi walivyopenda kuitwa mitume, ama, wamishenari badala ya mitume, sijui mimi. Lakini mmishenari lazima awe na wito wa Mungu na kutumwa na Mungu, “mtu aliyetumwa.”

⁹ Nabii ni mwonaji ambaye huiona mioyo ya watu na kutabiri mambo yatakayotukia. Na—na sasa, kuna karama ya unabii, iliyomo kanisani pamoja na washiriki wa mahali hapo, humshukia yeyote kati yao. Wanatoa unabii, basi hauwezi kupokewa kanisani mpaka upambanuliwe na mashahidi wawili au watatu, halafu, hawana budi kuweka muhuri wao juu ya huo, kusema ni wa Mungu, kisha inawabidi kuangalia waone kama utatukia. Basi huenda isimwangukie huyo ndugu au dada tena. Huenda ikawa juu ya mwingine. . . Hiyo ni karama ya unabii.

¹⁰ Lakini nabii, n-a-b-i-i, huzaliwa nabii, daima kutoka. . . iliamriwa hivyo kabla hata ulimwengu haujaanza. Mnaona? Sasa, chukua kama Yesu Kristo, Mfalme wa manabii, Alikuwa, kutoka katika bustani ya Edeni, ule Uzao wa mwanamke, Nabii. Naye Musa alizaliwa mtoto mzuri, nabii. Yohana Mbatizaji, mbona, Isaya alimwona miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa, na akasema yeye ni “sauti ya mtu aliaye nyikani,” miaka mia saba na kumi na miwili kabla hajazaliwa. Yereimia, Mungu alisema kabla hata hajaumbwa katika tumbo la mama yake kwamba alimjua, na kumtakasa, na kumweka kuwa nabii wa mataifa. Mnaona?

¹¹ Manabii wana Neno la Mungu, nao wanazaliwa nabii. Karama ya unabii ni tofauti, hiyo ni karama ambayo. . . sasa,

kuna tisa . . . kuna karama tano zilizowekwa Kanisani: mitume, manabii, walimu, wachungaji, wainjilisti. Sasa, hizo ni karama tano ambazo Mungu huweka Kanisani kwa kujua Kwake tangu zamani.

¹² Kisha kuna karama tisa zilizomo kwenye Kanisa la mahali hapo: kunena kwa lugha, kufasiri lugha, na karama za hekima, na maarifa, na—na unabii, na kadhalika. Hizi ni karama tisa za kiroho zinazofanya kazi kupitia Kanisa, lakini basi kuna tisa . . . karama tano za ofisi ambazo Mungu huweka Kanisani. Na, loo, jinsi tunavyopenda kuziona zote zikifanya kazi katika . . . Moja yazo ni mchungaji, mwalimu, na mambo hayo. Kisha hizo zingine zinafuata katika thibitisho. Karama ni za kukuza. Na Mungu ameziweka tu hivyo hata m—mpumbavu hatapewa udhuru, sivyo? Ataninii . . . Ni rahisi sana jinsi Mungu alivyofanya hilo. Nami napenda hilo.

¹³ Kadiri unavyokuwa rahisi, ndivyo utakavyokuwa mkuu zaidi mbele za Mungu. Hiyo ni kweli. Usijaribu kamwe kujiinua, unapofanya hivyo, unajishusha. Unaona? “Ajikwezaye atashushwa.”

¹⁴ Si muda mrefu uliopita nilikuwa . . . (Je, ninakosea hapa, Ndugu? Loo, asante, Ndugu. Vema. Hiyo ni bora zaidi.) Asante. Labda sikuwa nasikika vizuri, huko nyuma.

¹⁵ Kulikuwa . . . Hivi majuzi nilikuwa katika . . . Watu walikuwa wamenitumia barua, niende kwenye mkutano mkubwa sana katika jiji kuu nchini Marekani, Chicago, kwenye mkutano wa Kipentekoste. Vema, ni—ni—nisingeweza kwenda hata hivyo, lakini sikuwa nimeijibu hiyo barua, ndipo mtu huyo aliyekuwa msimamizi akanitumia neno, “Usije.”

Naam, nikawazia, “Naam, hilo ni sawa.”

¹⁶ Kwa hiyo basi wakamchukua mhudumu fulani mashuhuri aliyekuwa na jina kuu, na jamani, jinsi alivyokuwa mwalimu fulani mkubwa wa shule ya Biblia. Ndipo mtu huyo alipokuja usiku huo, alikuwa na kitabu kikubwa sana, kilikuwa na kurasa kadhaa, naye akatoa hotuba hiyo ya kiakili alipokuwa akiisoma kutoka katika kurasa hizo, na kukigeuza, mazungumzo mazuri sana ya kiakili. Mnaona?

¹⁷ Lakini hao watakatifu wa Mungu walitulia tu, hayakuwa yakikolea, yeye alijua hilo. Aliposimama, kifua mbele, ukosi uliopinduliwa, mwajua, na haya yote *yafanywayo*. Ndipo akagundua ya kwamba hilo halikuendana na watu wa Mungu. Na ndipo—ndipo alipoona hayaendani, basi alifunga tu vitabu vyake kisha akarudi chini huku ameinamisha kichwa chake, akiondoka kwa unyenyekevu sana.

¹⁸ Kulikuwa na mtakatifu mzee aliyeketi nyuma pembeni, akamgusa huyo mwingine, na kusema, “Kama angalipanda jinsi alivyoshuka, angalishuka jinsi alivyopanda.” Hiyo ni kama

kweli. Tujinyenyekeze mbele za Bwana. Hiyo ndiyo njia ya kuifanya.

¹⁹ Nami nilikuwa nikiwazia tu, nilipokuwa nimeketi pale nje, niliendesha gari humu na kumsikiliza Ndugu Borders akimalizia ujumbe wake, nilikuwa nikiwazia kuhusu... ndugu zangu Wahindi. Natumai hili ni sawa. Nakumbuka kule Phoenix, Arizona, tulikuwa na he—he—hema la sarakasi, nami nilikuwa na mkutano kule. Basi kulikuwa na M—Mhindi aliyeingia kutoka... Nafikiri alikuwa M—Mnavajo, naye akaingia, Mnavajo wa asili, mwajua, amejifunga ugwe wa bluu kichwani, na amevaa shati jekundu. Naye hakuketi kwenye kiti, aliketi tu papo hapo sakafuni. Mnaona?

²⁰ Na kwa hiyo mimi... Billy alikuwa akitoa hizo kadi za maombi, na kushuka, akizichanganya na kuwapa watu. Basi wakati angeweza... Watu walikuja jukwaani wakiwa na maumivu ya jino, na huyo mwingine alikuwa na, labda, angekuwa, mwajua, anaumwa na tumbo ama *kitu kingine*, kidogo, kitu kidogo.

²¹ Ndipo nikamwambia Billy, nikasema, “Mwanangu, acha kuwapa kadi watu wasio na chochote ila maumivu ya meno tu, wakati kuna watu wanaoketi hapo na kansa, wanakufa, hawana budi kuja jukwaani. Waulize hao watu wana shida gani na kisha uwape kadi ya maombi. Mtu fulani... Mpandishe huko mtu anayekufa, sababu wana usiku mmoja tu zaidi, nasi hatuna budi kufunga, na kuna yapata watu elfu tano kule wa kuombewa, na wao—wao ni wagonjwa kweli.”

²² Kwa hiyo Billy akasimama kwenye, kipaza sauti, akasema, “Baba alisema wapewe tu kadi hizi watu ambao ni wagonjwa sana.” Kasema, “Sasa, ninapokupa, unaniambia una shida gani nami nitakupa kadi.” Naye akasema, “Ni watu tu walio na maumivu ya meno, na kadhalika, na mambo kama hayo, madogo... wanaoumwa kidogo na kichwa...” Bila shaka hilo ni tatizo kubwa kwao, lakini si tatizo kama la mtu anayekufa, na ugonjwa wa moyo, au—au kitu kibaya sana.

²³ Kwa hivyo nitamwita “Chifu.” Alikuwa ameketi pembeni kwenye mavumbi sakafuni, ndipo akamwendea Billy, akampigapiga mgongoni, akanyoosha mkono wake.

Billy akasema, “Chifu, kuna nini?” Kasema, “Baba aliniambia niulize watu wana matatizo gani.”

Akasema, “Mimi mgonjwa.”

Akasema, “Kwani unaumwa wapi, Chifu?”

Akasema, “Mimi mgonjwa.”

Billy akasema, “Vema, si—sijui la kufanya.” Akasema, “Vema, kaa chini, nitakufikia katika dakika chache.”

²⁴ Akamwangalia, hayo macho madogo yakitazama. Wakati lundo hilo dogo la kadi lilipopungua sana, alisogea na kumgusa tena, naye akasema, “Mimi mgonjwa.”

²⁵ Na kwa hivyo Billy akasema, “Chifu,” kasema, “itabidi uniambie una shida gani. Baba alisema kadi hizi wapewe tu watu ambao walikuwa wagonjwa sana. Kwani una tatizo gani? Unaumwa wapi?”

Akasema, “Mimi mgonjwa.”

Billy akasema, “Sawa, Chifu, chukua hii na uandike juu yake ‘Mimi mgonjwa.’” Mnaona?

²⁶ Kwa hiyo ikawa, akaingia kwenye mstari wa maombi usiku wa pili, kesho yake usiku. Kwa hiyo akaja pale, bila shaka Bwana akaanza kunena, akieleza shida na chochote kile, na kadhalika.

Na kwa hiyo nikasema, “Chifu?”

“Naam?”

²⁷ Nikasema, “Unaamini Bwana atakuponya?” Akanitazama. Nami nikaona hakulipata vizuri sana. Mnaona? Nikasema, “Je, unaamini Bwana atakuponya?”

Akasema, “Hiyo kweli.”

Nami nikasema, “Je, utakuwa mvulana mzuri baadaye?”

Akasema, “Hiyo kweli.” Na kila kitu nilichomwambia, alisema, “Hiyo kweli.”

²⁸ Kumbe, kulikuwa na maneno mawili pekee angeweza kunena, alikuwa amejifunza hayo “Mimi mgonjwa” na “Hiyo kweli.” Nilikutana naye yapata, loo, miezi sita ama minane baadaye kule chini, nikasema, “Yule pale yule ndugu wa Kihindi.” Nikamwendea. Nikasema, “Habari yako Mwenzangu?” namna hiyo.

Yeye kasema, “Hiyo kweli.”

²⁹ Mtu fulani, mmishenari huko nje alisema aliponywa. Mnaona? Aliponywa. Na hayo ndiyo yote aliyojua, “Hiyo kweli.” Kwa hiyo... Hayo ndiyo yote unayopaswa kujua, “Hiyo ni kweli.” Kwa hiyo tunashukuru sana kwa ajili ya imani hiyo rahisi. Kitu pekee unachopaswa kujua ni, “Hiyo ni kweli,” tunapozungumza kuhusu Biblia. Hiyo ni kweli.

³⁰ Mchina wakati mmoja, kunaweza kuwa na Wachina hapa usiku wa leo, alisema, “Nye Wamarekani hamsomi vizuri.” Kasema, “Nyote mnasoma kuingama ukurasa *hivi*.” Kisha kasema, “Nitakusomea Yohana 3:16.” Akasema, “Ninyi husema, ‘Mungu aliupenda sana ulimwengu, akamtoa Mwanawe wa pekee, kila amwaminiye, asipotee. . .’” Kasema, “Mnasema, ‘La, la, la.’” Kisha kasema, “Sisi Wachina, tunasoma juu chini kwenye ukurasa, ‘Mungu aliupenda sana ulimwengu, akamtoa Mwanawe wa pekee. . .’” Hiyo kweli. Hiyo kweli.

³¹ Nikizunguka kote, nikikutana na watu mbalimbali katika mataifa mbalimbali, inashangaza sana, lakini kujua watoto wote wa Mungu ni watu wa ajabu. Haijalishi ni lugha gani, kile walicho, wote ni watoto wa Mungu, na wazuri sana, nami na—nawapenda wote. Wanorwe, Waswidi, na Wafini, na huko Ufini, huko ndiko yule mvulana mdogo alikofufuliwa katika wafu. Labda mliisoma hiyo hadithi huko. Na hiyo ni mara tano moja kwa moja, kwa uchunguzi wa madaktari, ambapo watu watano, wakiwa wamekufa, kwa neema ya Mungu, kupitia ono, walirejeshewa uhai wao tena. Na hizo ni taarifa za madaktari zilizoidhinishwa. Mnaona?

³² Mlisoma hilo katika Wafanyabiashara Wakristo si muda mrefu uliopita kuhusu mtoto mchanga wa Kimeksiko? Sasa, vile...Mnaona, kabla ya kuchapisha lolote katika magazeti unapaswa kuwa na uwezo wa kulithibitisha. Unaona? Unaweza kulisema, hilo ni sawa, maana unaweza kulikana, lakini unapolichapisha, afadhali uliweke sawa. Na kwa hiyo mtoto huyu mdogo wa Kimeksiko, daktari alitia sahihi ya kwamba alikuwa amekufa asubuhi hiyo huko Meksiko. Kulikuwa na maelfu...Vema, wito mmoja wa madhabahuni uliwaleta watu elfu ishirini kwa wakati mmoja. Ndipo mtoto huyu mdogo wa Kimeksiko...

³³ Sasa, wote walikuwa Wakatoliki, nao walikuwa...Loo, ni ninii sana...Ninii tu...Walikuja huko saa tatu asubuhi, na kungoja mpaka nilipofika huko saa tatu usiku huo, wakingoja, nije. Nami nikaja jukwaani. Mvua ilikuwa ikinyesha siku nzima, ikimwagika tu, nao wakasimama pale pale, moja kwa moja kwenye mvua hiyo.

³⁴ Usiku uliotangulia huo kulikuwa na ndugu mzee wa Kimeksiko, akaja jukwaani, hana viatu miguu, suruali imechakaa kabisa, kofia kuukuu iliyoshonwa kwa ugwe wa kitani. Naye alikuwa akija kupitia jukwaani, akitetemeka, namna *hiyo*, ndipo akaingiza mkono mfukoni mwake na kutoa...baadhi ya shanga za kukariri “Salamu Maria,” nami nikasema, “Hiyo haihitajiki.” Mkalimani, Ndugu Espinoza... Baadhi yenu watu wa Assemblies of God mnaweza kumjua Espinoza. Yuko pamoja na...Na kwa hiyo alikuwa mkalimani wangu. Naye...Nikasema, “Hiyo haihitajiki.”

³⁵ Kwa hiyo akaja, nami nikatazama, nami huyo hapo, nimesimama hapo nimevaa jozi nzuri ya viatu, suti nzuri aliyonipa mtu fulani. Naye huyo hapo maskini huyo ndugu mzee, hakuwa na viatu, hakuwa na suti, koti lake lilikuwa limechakaa, hana shati kabisa, amejaa mavumbi. Labda, maskini mzee huyo hakuwahi kupata mlo mzuri maishani mwake, nami ndiyo kwanza nimalize kula chakula kizuri.

³⁶ Pia kumbukeni, yeye ni—yeye ni mtu ambaye Kristo alimfia, sawasawa na mimi, ama mtu mwingine yeyote, yuna haki tu

kadiri nilivyo nayo. Labda kundi la watoto wadogo nyumbani, au labda vijana wakati huo, maana angekuwa ni kama rika ya baba yangu, na huyo hapo kipofu kabisa.

³⁷ Ndipo nikaweka mguu wangu kando ya wake, kusanyiko lisingeweza kuona hilo. Loo, hilo jukwaa lilikuwa refu kadiri jengo hili lilivyo pana, basi nikaweka kiatu changu kando ya mguu wake nione kama kingemtosha, ningempa viatu vyangu, nami nikawazia hilo, lakini miguu yake ilikuwa mikubwa zaidi.

³⁸ Kisha nikayalinganisha mabega yangu na mabega yake, koti langu lisingemwenea. nikawazia, “Ee Mungu, hilo hapo.” Ndipo nikaona nywele zake zenye mvi zikining’inia chini, macho yake meupe, nikawazia, “Laiti ningeweza kumsaidia kwa njia fulani.” Huna budi kuwahurumia watu, la sivyo hutawafaa kitu unapowaombea, huna budi—huna budi kuwahurumia. Nikawazia, “Vipi kama baba yangu angeishi? Angekuwa na umri kama huo, labda yeye ni baba wa mtu fulani.”

³⁹ Nami nikawazia, “Halafu basi, wazia tu kwamba Shetani amekuwa mwovu sana kwake. Maumbile yamemweka katika hali aliyo ndani yake, pengine, katika hali hii ya ufukara, na hapa hata hana macho ya kuona apate kutembelea.”

⁴⁰ Basi nikamkumbatia maskini jamaa huyo, nami nikasema, “Baba wa Mbinguni, ninamwombea mzee huyu mpendwa.” Nikamtazama, amesimama hapa nje katika ono, mbele yangu, angeweza . . . akinitazama moja kwa moja. Loo jamani, hakuna kitakachozuia hilo wakati ono hilo linapotokea. Naam, bwana.

⁴¹ Nikaona aliweza kuona, nikamsukuma tu kutoka kwangu namna *hiyo*, naye akapaza sauti, “Gloria a Dios!” Hiyo inamaanisha “Utukufu kwa Mungu.” Hapo angeweza kuona vizuri kadiri nilivyoweza. Basi kesho yake usiku kulikuwa na lundo la shela kuukuu na kofia ambazo zilikuwa kama futi tatu kwenda juu na karibu—karibu urefu wa yadi kumi na tano, ishirini. Jinsi wanavyojua ni ya nani, sijui, zimekundikwa tu pamoja zipate kuombewa.

⁴² Nilipofika jukwaani, Billy, mwanangu, aliniambia . . . Tulikuwa ndio kwanza tumeanza kuhubiri. Ndugu Espinoza . . . Nikapanda juu . . . mimi . . . Tulikuwa tu na siku tatu usiku, zote tungeweza kuwa huko. Nami nikasema, “Sasa, nitazungumza usiku wa leo, kama nilivyofanya jana jioni, kuwaambia nyote kile Yesu alichokuwa, nanyi mlimwona hapa akipitia kwenye kusanyiko, mkamwona akiyafungua macho ya vipofu. Tazameni, yamewekwa pale, lundo kubwa la magongo ya kale, na viti, na viti ambavyo watu walikalia.”

⁴³ Nikasema, “Inaonyesha kwamba imani yao katika Bwana aliyefufuka imefanya hivi.” Nami nikasema, “Basi, imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.”

44 Ndipo Billy akanijia, akasema, “Baba, nina karibu mabawabu mia tatu upande *huu*,” kisha akasema, “hawawezi kumzuia mwanamke mdogo.” Kisha kasema, “Yeye ana urefu karibu *hivi* tu, mwanamke mchanga,” kasema, “ana mtoto mchanga aliyefariki, naye amekuwa akisimama kwenye mvua hiyo huko nje.” Kisha kasema, “Mañana kamwe hakumpa. . .”

45 Mañana, neno *mañana* linamaanisha “kesho,” naye alikuwa mwenda pole sana hata nikamwita “kesho.” Mnaona? Alipaswa kunijia, wanasema saa kumi na moja, na alifika pale kama saa mbili na nusu ama tatu. Mnaona? Ndipo nikamwita Mañana.

46 Akasema. . . Alikuwa akisambaza kadi za maombi, ilimbidi Billy kuangalia kwamba hakuuza yoyote. Mnaona? Hilo ndilo tunalopaswa kuangalia, sio. . . Mtu anayesambaza kadi za maombi ana jukumu kubwa, na hiyo ndiyo sababu nina mwanangu mwenyewe akizisambaza, maana watu. . . jambo baya lingetukia. Na kwa hiyo basi, alimwanguka tu, naye akazisambaza hizo kadi za maombi.

47 Basi akasema, “Amesambaza kadi zote za maombi, naye maskini mwanamke huyu hakupata yoyote.” Kisha kasema, “Watu hao wamekuwa wakisimama. . .” Kwa kadiri ulivyoweza kuona mbali kuzunguka uwanja huo wa michezo ya ng’ombe kule, pamoja na. . . wamesimama hapo siku nzima, tangu saa tatu, ama, mbili, au saa tatu asubuhi hiyo, walipoyafungua hayo malango, na hii ilikuwa yapata saa tatu na nusu usiku huo, labda saa nne kasorobo.

48 Kisha akasema, “Naye maskini mwanamke huyo amepanda kupitia kwa mabawabu hao, ana mtoto mchanga aliyefariki amefunikwa kwa blanketi, anataka umwombee.” Kisha kasema, “Anapanda juu ya mabega yao, anakimbilia katikati ya miguu yao.” Naye akasema, “Inatubidi tu kurudi kule na kumwondoa jukwaani,” mnaona, kwa maana siwezi kumwacha aje hapa bila kadi ya maombi, maana itasababisha ghasia, unaona, maana hao watu walisimama hapo muda huo wote wakingojea kadi ya maombi.

49 Naye Ndugu Jack Moore, wengi wenu nyote huenda mnamfahamu, kutoka Shreveport, Louisiana, huenda baadhi yenu mmesikia habari zake, yeye ni mtu mzuri sana, alikuwa jukwaani pamoja nami, nikasema, “Ndugu Moore, mwanamke huyo asingenitambua. Nenda pale ukamwombee huyo mtoto, popote alipo, wala hatajua tofauti.”

Akasema, “Sawa, Ndugu Branham.”

50 Akaanza kwenda, nami nikasema, “Sasa, Ndugu Espinoza, tafsiri.” Nikasema, “Kama nilivyokuwa nikisema, ‘Imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni. . .’” Nami nikatazama, na papa hapa, mbele yangu, kulikuwa na mtoto mchanga wa Kimeksiko ameketi pale. Ilikuwa ni uso mdogo

wa hudhurungi, naye alikuwa akicheka nami, hakuwa na meno yoyote, fizi zake ndogo tu zikionekana, papa hapa mbele yangu.

⁵¹ Nikawazia, “Sijui kama huyo ndiye mtoto huyo.” Nami nikasimama, nikasema, “Usitafsiri.” Nikasema, “Ndugu Moore, ngoja kidogo.” Nikasema, “Billy, tengeneza njia ukamlete mwanamke huyo hapa, jukwaani.”

⁵² Na kwa hiyo wakamleta maskini mwanamke huyo, naye akaja, akapiga magoti, akaanza kupiga kelele, “Padre! Padre!” Hiyo inamaanisha “baba,” alikuwa Mkatoliki, unaona, “Padre! Padre!”

⁵³ Nami nikamshika mkono, nikasema, “Simama, simama.” Naye akamshika mtoto—mtoto wake mchanga aliyekauka, mrefu *hivi*, chini ya blanketi, amelowa tu maji. Loo, mvua ilikuwa ikinyesha tu siku nzima, na kulikuwa kumelowa kabisa. Nami nikasema, “Unajua Kiingereza?”

Naye akaendelea tu kusema, “Padre! Padre!” Naye Ndugu Espinoza akamwambia anyamaze.

⁵⁴ Na kwa hiyo nikaweka mkono wangu juu ya, maskini blanketi dogo namna *hiyo*, maskini mwili huo mgumu, baridi. Nikasema, “Baba wa Mbinguni, sitaki... Ninajua huna haja ya kuponya ili kujithibitisha Mwenyewe, Wewe huponya ili kulitimiza Neno Lako.” Nikasema, “Sote tunajua ya kwamba Wewe ni Mungu, lakini muda mfupi tu uliopita ono lilikuja mbele yangu, kama ujuavyo, mtoto mchanga. Je, ilikuwa ni mtoto huyo, Baba? Endapo siye...”

Yapata wakati huo, akafanya “Waai, waai,” akaanza kurusha mateke yake madogo namna hiyo, na hapo akawa hai. Ndipo basi...

⁵⁵ Kwa hiyo nikamwambia Ndugu Espinoza, nikasema... Naye akaanza tu kupiga mayowe na akaanguka chali namna *hiyo*. Na—na kwa hiyo nikasema... Mama mdogo mrembo, msichana mdogo tu, labda katika miaka yake ya ishirini, labda ni mtoto wake wa kwanza.

⁵⁶ Na kwa hiyo nikasema, “Ndugu Espinoza, sasa, usiseme lolote kuhusu hilo sasa. Mnaona? Kwa sababu, jambo la kwanza, weka mkimbaji pamoja na huyu mtoto mchanga, upate kujua kutoka... Acha daktari wake atie sahihi taarifa. Mnaona? Maana hatutaki kitu ambacho...” La—lazima iwe ni kweli. Mnaona? Hutaki chochote... Mtu akisoma chochote, unataka kiwe ni kweli, lisiwe ni jambo baya, kwa sababu hilo lisingekuwa sawa mbele za Mungu.

⁵⁷ Na kwa hiyo, akaenda, naye huyo daktari akatia sahihi taarifa ya kwamba huyo mtoto alikufa kwa nimonia, asubuhi hiyo, saa tatu ofisini kwake. Na hiyo ilikuwa saa nne, kama saa nne usiku huo, alikuwa amekufa wakati huo wote, naye anaishi huko Meksiko leo hii, mzima na mwenye furaha, mnaona,

kwa sababu Kristo yu hai, Kristo yu hai. Basi inahitaji nini? Imani rahisi.

⁵⁸ Nilimwambia mchungaji wenu, Ndugu Eddie Byskal, Nilimwambia usiku wa leo, ama, alasiri ya leo nilipokuwa nikizungumza naye, nikasema, “Ni vibaya sana kwamba hatukuwa na wiki sita kamili,” tumekuwa tukija pwani, “kuwa mumu humu miongoni mwa watu.”

⁵⁹ Akasema, “Ndugu Branham,” kasema, “hiyo si theluthi moja ya Wahindi,” akasema, “wao ni wavuvi wa kibiashara, na wote wako huku nje kwenye visiwa hivi na nje kupitia huko.”

⁶⁰ Nikasema, “Loo, jamani. Jinsi ningependa kuingia kwenye mashua ndogo na kwenda kisiwa kwa kisiwa miongoni mwao.” Isitoshe, bali niliona jana usiku, mkutanoni, baadhi yenu ninyi Waswidi, na Wanorwe, na Wajerumani wanaoketi huko nyuma, Wakanada, imani ya ajabu. Mungu awabariki. Ninyi ni watu wa ajabu. Tunaye Mwokozi mkuu ambaye anatupenda sisi sote.

⁶¹ Nami ni—niko hapa... Nisingeweza kuwaponya, kama ningeweza kuwaponya, ningefanya hivyo, mnaona, mna jua ningefanya hivyo. Kama ningeweza kuchukua... Kama kuwaponya, kama ningeweza kuchukua ro—robo, senti ishirini na tano, na kuiweka chini, na kuisukuma huku na huku kwenye barabara hii, siku nzima, kwa pua yangu, kisha niwaone mkiponywa, ningefanya hivyo. Sasa, Mungu anaujua moyo wangu, hii *hapa* Biblia, na hiyo ni kweli, ningefanya hivyo. Lakini hilo halingefaa kitu. Mnaona? Lakini... Na sasa kama mtu atakuja na kusema, “Naweza kukuponya,” usiamini hilo, unaona, kwa sababu hata dawa haiponyi. Mungu ndiye Mponyaji pekee aliyepo, “Mimi ni Bwana, Mungu wenu, niponyaye magonjwa yenu yote.”

⁶² Wakati mtoto huyu Mkanada, Donny Morton, mlisoma hiyo hadithi katika *Reader's Digest*, walipomleta mpaka kule chini, mwenye kifafa sana na amepindika hata Johns Hopkins, Mayo Brothers, na wote, wakamkataa. Ndipo akashuka hadi Costa Mesa, naye alikuwa mkutanoni, kisha Roho Mtakatifu akanena. *Reader's Digest* iliandika, kasema, “Huyo,” kasema, “Huyo mwinjilisti hakumwuliza mvulana huyo, alimwambia mvulana huyo yeye ni nani, akamwambia aliyokuwa amefanya, na alikotoka, na ni nini kuhusu hayo, naye akaponywa,” mnaona.

⁶³ Ndipo basi nikaitwa huko kwa Mayo Brothers kwa ajili ya, mahojiano ya hilo, nao wakasema... Nikasema, “Vema, mimi...” Hawakuwahi kuweka jina la Mayo Brothers hapo, lakini wao... hapo walikuwa na *Reader's Digest*, naye baba ndiye alikuwa amesema hivyo, lakini bila shaka mwandishi hangesema hivyo kuhusu ho—hospitali, na yale iliyosema.

⁶⁴ Ninii nyingi kubwa... Kama ulisoma makala hiyo, ilisema kliniki nyingi kubwa kote Marekani na Canada zilikuwa zimemkataa, na kifafa, amepindika, jina lilikuwa Donny

Morton, *Reader's Digest* ya Oktoba, yapata miaka minne iliyopita. Na kisha, akasema huyu mto- . . . mvulana huyu mdogo mwenye umri wa miaka minane hivi . . .

⁶⁵ Loo, ni hadithi ya kuhuzunisha, jinsi maskini ndugu huyu wa Canada alivyoshuka kwenye sleji. Alisema alijua baadhi ya wasichana viziwi na mabubu walioletwa kwenye mkutano wangu kabla ya hapo, na Bwana akamponya mmoja. Na mmoja wao ni mwimbaji kanisani, na huyo mwingine ni opereta wa simu. Kwa hiyo wote wawili walikuwa viziwi na bubu.

⁶⁶ Kwa hivyo akasema, "Hatujashindwa, Donny. Twende na . . ." Inaeleza . . . Naye mama na hao wengine walidhani labda wangeweza kuchukua dola hamsini, nao wote wakaja Marekani, na kumpeleka Donny mkutanoni, na chochote kile. Hazitalipia hata moja ya safari zao kwenye ndege. Ilibidi waje kwa basi, hata hawageweza kuja kwa gari moshi, basi walipofika kule, iliwabidi kuchukua Msaada wa Wasafiri wapate kufika kule, mahali mkutano ulipokuwa.

⁶⁷ Ndipo Roho Mtakatifu akamwambia yeye alikuwa ni nani, alikotoka, na kadhalika, maskini baba mdogo aliyejikunyata, akiwa amemshika mtoto wake mchanga. Na kwa hiyo . . . Kisha akamwambia yale hasa yangetokea. Bwana akamponya huyo mtoto kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Nao wakihojiwa juu ya hilo, walisema kwenye Mayo Brothers, "Kasisi Branham, hatudai kuwa waponyaji, tunadai tu kusaidia maumbile, kuna Mponyaji mmoja, huyo ni Mungu." Hiyo ndiyo bora zaidi, sivyo. Mnaona?

⁶⁸ Daktari anaweza kuunganisha mkono mahali ambapo umevunjika, lakini hawezi kuuponya. Daktari anaweza kung'oa jino, lakini hawezi kuponya mahali lilipotoka. Anaweza kukata kidole tumbo, lakini atakayeponya ni nani? Mnaona, hakuna dawa ambayo itajenga seli, seli ni—ni ukuaji. Mnaona? Wala hakuna kitu kinachoweza kuuponya huo, hakuna mtu awezaye. Na kuwa na uvimbe ni uzidishaji wa seli, ambao ni uumbaji, na kuna Muumba mmoja, ambaye ni Mungu. Mnaona? Naye hana budi kuunganisha mahali hapo, kuuweka mfupa huo pamoja. Daktari anaweza kuuweka vizuri, lakini, mnaona, wao . . . inabidi . . . Inahitaji kalisi, potashi, na kadhalika, kuingia kwenye mfupa huo kuuunganisha pamoja.

⁶⁹ Sasa, kama nilikuwa nikiliwasha gari langu hapa nje, ama nikishughulika nalo na nikauvunja mkono wangu, nami nikakimbia kwa daktari, kasema, "Dak, wewe ni mponyaji, uponye mkono wangu haraka sana, nataka kulimalizia gari langu."

Angesema, "Unahitaji uponyaji wa akili ewe mvulana." Hiyo ni kweli.

"Vema, ikiwa wewe ni mponyaji, uponye mkono wangu." Yeye si mponyaji. Mnaona?

Anasema, “Ninaweza kuuweka mkono wako vizuri, Mungu hana budi kuuponya.”

⁷⁰ Kwa hiyo basi... Mnaona? Maandiko sikuzote ni ya kweli “Mimi ni Bwana, niponyaye magonjwa yenu *yote*.” Hiyo ni kweli. Tunashukuru kwa ajili ya hospitali, na dawa, na kadhalika, zinasaidia maumbile, lakini haziponyi. La, wao si waponyaji, Mungu ndiye Mponyaji, Maandiko hayawezi kusema uwongo. Mnaona?

⁷¹ Sasa, nadhani hiyo ndiyo sababu ninachukua muda mwingi sana, ninyi ni wazuri sana, naweza tu kusimama, kuzungumza nanyi, na jambo ndilo hilo. Lakini mnajua nini? Sininii... Ninapita tu wakati huu, sina ila muda mfupi tu wa kukaa nanyi. Lakini nataka kufanya miadi pamoja nanyi. Je, ninaweza kuifanya, ninyi nyote? Tukiisha kuuvuka ule mto, ng'ambo ya pili, na tutakuwa vijana wa kiume na wa kike tena, nataka—nataka miaka elfu moja ya miadi na kila mmoja wenu.

⁷² Tuketi kando ya miti isiyokauka, na kuketi pale na kuzungumza, ndipo hapo atakuja Ibrahimu, nasi tutasimama na kupeana mikono na Ibrahimu, na Danieli atakuja hapo nasi tutapeana mikono naye, na kuruka-ruka, kupaza sauti kidogo, na kuketi chini tena, na kuzungumza tu kuhusu Port Alberni tulipokuwa na mkutano hapa. Sasa, hiyo inasikika kama, kwa watu wengine, inaweza kuwa ni hekaya, lakini hiyo ni kweli. Amina. Hiyo ni kweli iwezavyo kuwa.

⁷³ Sasa, kabla hatujawaombea wagonjwa, ama lolote tufanyalo... Na sasa, ninawatakeni mjue kwamba uponyaji wa Kiungu, hatujaribu kuufanya huo kizingiti chetu kikuu. Daktari F. F. Bosworth, rafiki msiri wangu, ameenda Mbinguni hivi majuzi, mzee kwelikweli, wengi wenu mmesikia habari za Fred Bosworth, alikuwa mzee mtauwa, mtakatifu, naye alisema, “Uponyaji wa Kiungu ni kama tu kwenda kuvua samaki,” kasema, “kamwe humwonyeshi samaki ndoano, unamwonyesha chambo. Ananyakua chambo na kupata ndoano.” Kwa hiyo hiyo ni... .

⁷⁴ Kwa hiyo—kwa hiyo yapata asilimia themanini na sita ya huduma ya Yesu ilikuwa juu ya uponyaji wa Kiungu, unavutia usikivu, wa kitu fulani cha Kimbinguni kinachofanyika, ndipo watu basi wanamwamini Mungu mwenye nguvu, anayefanya jambo hilo, mnaona. Kwa hiyo uponyaji wa Kiungu ni jambo dogo, na kamwe huwezi kulifanya kubwa jambo dogo. Hiyo ni kweli, Bibi Byskal, sivyo? Hiyo ni kweli. Huwezi kulifanya kubwa jambo dogo.

⁷⁵ Kwa hivyo inatubidi kukumbuka kuwa hiki hapa ni kitu tu... Sasa, njia yangu halisi ya kuliona... Sasa, tunao watu mashuhuri ulimwenguni siku hizi, watu mashuhuri, Tommy Osborn, na—na (Loo, akina nani wote?), Oral Roberts, na hao watu, na mnao watu mashuhuri huku Canada, wanaopita,

wakiponya kwa maombi, wakiwawekea wagonjwa mikono. Loo, ninaheshimu hilo. Loo, jamani. Wao ni watu wa Mungu, imani kuu ya kushikilia.

⁷⁶ Lakini mtu fulani aliniandikia barua, miaka kadhaa iliyopita, nilipoanza kwa mara ya kwanza, akasema, “Ndugu Branham,” ukosoaji mzuri, nami ninauthamini huo, unakufanya ujue mahali unaposimama, maadamu watu hawawi, mwajua, loo, wabaya sana kuuhusu, wanataka tu kuwa ndugu na kukwambia unapokosea, nami ninathamini hilo. Sikuzote napendezwa na ukosoaji, maadamu ni—ni mzuri. Ndipo basi, mtu huyu akasema, “Unajua, Ndugu Branham,” akasema, “Oral Roberts atawaombea mia tano huku wewe ukiwaombea wawili.” Akasema, “Wewe ndiwe mtu mwenda pole sana niliyepata kumwona.”

“Vema,” nikasema, “hiyo—hiyo ni kweli,” nikamwandikia kumjibu.

⁷⁷ Lakini akasema, “Ndugu Roberts anaweza kusimama pale juu, na kuwawekea mikono namna *hiyo*, na kuwaombea wanapopita, na kuwaombea namna *hiyo*, nawe huyu hapa ungali umesimama hapo ukimshughulikia mmoja.” Mnaona?

⁷⁸ Nikasema, “Lakini unaona, Mungu alimpa Ndugu Oral Roberts njia ya kuwaombea wagonjwa, kisha akanipa njia nyingine ya kuwaombea wagonjwa. Naye Ndugu Oral Roberts anafanya hivyo kwa njia yake aliyoambiwa na Mungu, mimi ninafanya jinsi Mungu alivyoniambia.” Hiyo ni kweli.

⁷⁹ Nikasema, “Sasa, hivi ndivyo ilivyo, unapotafuta... Vipi, kwa mfano, kama una imani kubwa,” Acha tu niseme jambo fulani. Kwa kawaida, wale wanaokosa huja humu. “Sasa, tuseme kwa mfano, tuna imani kubwa, na huyu hapa mtu mmoja amesimama jukwaani, akiwa na wakati mzuri sana akipaza sauti, na utukufu wa Mungu uko hapa.” Nami nikasema, “Sasa, labda mtu huyu aliiba pesa, aliishi vibaya, labda alizurura na mwanamke fulani kwa uzinzi, ama alifanya mauaji ama jambo fulani, hata Mungu akaweka ugonjwa huu juu yake.” Mnajua, Mungu hutumia magonjwa kama viboko kuturudisha Kwake. Mnaamini hilo? Hakika ndivyo, ninii... mtazame Ayubu, kurudiwa na Bwana.

⁸⁰ Sasa, inabidi utambue, karama za kinabii zinaweza kukuingiza katika shida. Hakika zinaweza. Sasa, vipi kama mtu huyu amefanya jambo baya, nami nimesimama pale, imani kubwa sana, ile tunayoita Marekani, imani kakamavu isiyolegea, na nikamshika na kusema, “Haleluya, haleluya! Shetani mwachilie. Utukufu kwa Mungu,” na niondoe ugonjwa huo kwake, huku Mungu aliuweka juu yake kwa kusudi fulani? Nina shida na Mungu. Mnaona ninalomaanisha?

⁸¹ Labda hamlipati. Ngojeni, hebu niwape Maandiko machache, najua hamtayatilia shaka Maandiko. Hapa, hebu

tumchukue Musa. Ni wangapi wanaamini Musa alikuwa nabii, nabii mkuu? Mungu alimwambia Musa, “Shuka kule chini ukaseme na mwamba.” Ndipo Musa akashuka akaenda kule na kufanya kile ambacho Mungu alimwambia asifanye, aliupiga mwamba. Aliupiga mara ya kwanza, lakini Mungu alimwambia aseme nao, nao huo mwamba ulikuwa ni Kristo. Alipigwa mara moja, ilinena juu ya—ya udhaifu wa Damu ya Kristo basi, kwenye... Naye Musa akaupiga mara ya kwanza, maji yakatoka, kisha wakalia tena, na kuendelea kulia wapate maji zaidi na kitu kingine, ndipo Mungu akamwambia ashuke akaseme na huo mwamba.

⁸² Lakini akaupiga, maji hayakutoka, naye akaupiga tena. Alikuwa na nguvu za kufanya jambo hilo, alikuwa nabii. Nayo maji yakatoka. Hiyo ni kweli. Mungu alifanya nini? Kasema, “Njoo huku, Musa.” Kasema, “Unaiona ile nchi huko ng’ambo? Hutaingia, hukunitii Mimi kule chini kwenye mwamba.” Mnaikumbuka hiyo hadithi, sivyo? Alikuwa na uwezo wa kufanya jambo hilo, lakini afadhali aangalie jinsi alivyotumia nguvu hizo.

⁸³ Mwangalie Eliya, alikuwa na upara, naye alikuwa akishuka kuja njiani, ndipo watoto wengine wadogo wakaanza kusema, “Mzee kipara, mzee kipara, kwa nini usipande juu kama—kama Eliya alivyofanya?” wakimdhihakiki. Sasa, hiyo ilikuwa ni sawa, hao watoto wadogo, hawakuninii... labda—labda wazazi wao ndio waliowafundisha kufanya hivyo, walikuwa ni jamaa wadogo. Walikuwa wakimdhihakiki nabii huyu, lakini wakamkasirisha, naye akageuka na kuwalaani watoto hao, katika Jina la Bwana, ndipo dubu wawili wakatoka msituni na kuwaua watoto arobaini na wawili wasio na hatia.

⁸⁴ Sasa, hilo halisikiki, tabia ya Roho Mtakatifu, sivyo? Hapana, kuwaua hao watoto wadogo. Mnaona? Lakini nabii mwenye hasira! Mnaona? Aliwalaani hao watoto, ilimbidi kutambuliwa, kwa maana yeye alikuwa nabii. Mnaona? Kwa hiyo huna budi kuangalia.

⁸⁵ Angalieni, katika mstari huo, naona kilicho shida ya mtu huyo, nawaambia, kisha naangalia, nione kile watakachosema au kufanya; nione kile Yeye anachoniambia nifanye. Ikiwa kuna kitu kibaya hapo, bado inabaki nyeusi na giza na baridi, nasema, “Nenda, na Bwana akubariki.” Lakini basi kama sivyo, na ninaona inatendeka, ninawaona siku za usoni, basi ninasema, “BWANA ASEMA HIVI,” mnaona. Ndipo mnaona yote ni sawa basi, yatatendeka.

Sasa, ombeni tu, aminini, na siku moja natumaini kurudi pamoja nanyi, ili tuweze kukaa pamoja kwa muda mrefu, basi, Bwana akipenda.

⁸⁶ Sasa, ninataka kusoma fungu dogo la maneno linalojulikana kutoka katika Maandiko, nalo linapatikana katika Mathayo

Mtakatifu katika mlango wa 12, na tuanzie kwenye kifungu cha 41.

Nao watu wa Ninawi watasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, nao watawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu walitubu kwa mahubiri ya Yona; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Yona.

Naye malkia wa kusini atasimama katika kiza-... katika hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.

⁸⁷ Sasa, ningetaka kuchukua kama somo: *Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa. Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa.* Na kwa ajili ya fungu, “Kuzitambua Karama Na Ishara za Mungu.” Sasa, na tuombe.

⁸⁸ Baba yetu wa Mbinguni, ndio kwanza tusome kutoka kwa Neno Lako, Nawe ni Neno, na sikuzote umekuwa ni Neno. Na sasa, tunakushukuru ya kwamba tuna imani ya kujua na kuamini ya kwamba kila kitu kinakwenda sawasawa na ratiba. Usiku wa leo, mkutano huu uko kwa wakati wake kabisa, na ulimwengu na mafanikio yake yote yako kwenye wakati wake hasa.

⁸⁹ Na, Ee Baba, nilipopitia kwenye Maonyesho ya Ulimwengu siku chache zilizopita, nikiangalia mafanikio ambayo mwanadamu amepata, na jinsi alivyoendelea. Jinsi watu walivyokuwa wamekusanyika kutoka ulimwenguni kote kuona kile ambacho ulimwengu ulikuwa unafanya, wakitafuta yaliyo bora sana ambayo wamefanya, Ujerumani, Uingereza, Uswisi, ulimwengu wote ulikuwa ukionyesha kile ambacho wameweza kuboresha.

⁹⁰ Na halafu, Bwana, tunakuja kwenye mji huu mdogo, huko nyuma kabisa kule kwenye Port Alberni, ambapo baadhi ya Wahindi waliojitenga kutoka kisiwani, wanaojua maana ya kumshukuru Mungu kwa ajili ya kuvua samaki wengi, waaminifu na wakweli, ambao wanaweza kusimama mlimani na kutazama machweo ya jua na kulia, kumsifu Mungu wakati ndege wanapoamka asubuhi na kuanza kuimba, nao wanaweza kumwona Mungu katika maumbile, na kumsikia akilia katika shakwe, na kumwangelia akipiga mbawa zake kubwa hewani.

⁹¹ Lakini tumekusanyika hapa kwa ajili ya maonyesho ya ulimwengu wa kiroho, kuona yale Mungu ameweza kufanya na Kanisa Lake katika wakati wote, jinsi amekuwa kutoka—kutoka kwenye maungamo hadi karama, na ishara, na kunena kwa lugha, na maajabu, na sasa moja kwa moja hadi kwenye ishara ya mwisho. Mungu katika mambo yake makuu, akiuonyesha ulimwengu yale ambayo ameweza kufanya na watu Wake. Nasi

tunafurahi sana kuwakilishwa usiku wa leo, Bwana, miongoni mwa kundi la watu ambao... wanaamini, na ni waaminifu, na husafiri kila mahali kutafuta wema wa Mungu.

⁹² Sasa, Baba wa Mbinguni, libariki Neno Lako, wabariki watu Wako kila mahali. Waokoe waliopotea, Bwana, Ee Mungu, hawana budi kwenda siku moja, tunajua.

⁹³ Nami natumaini, Bwana, ya kwamba usiku wa leo, itakuwa kwamba tutakuwa namna ya watu wa Mataifa ambao Yesu alipendezwa nao. Tunasoma katika Biblia ambapo Yairo, msichana wake mdogo alilala akiwa mgonjwa, akifa, naye akasema, "Njoo, uweke mikono Yako juu ya mtoto wangu, naye atapona." Lakini wakati yule Mrumi, Mmataifa, yeye alisema, "Sistahili Wewe uingie chini ya paa langu. Sema tu Neno, na mtumishi wangu ataishi." Ndipo basi ukageuka, ukawatazama Israeli, ukasema, "Sijapata imani kama hiyo katika Israeli."

⁹⁴ Sasa, Baba, hatujaribu kuweka mikono juu ya wagonjwa, ili nikiondoka waseme kwamba "ndugu *fulani* alipitia hapa na kuniwekea mikono." Lakini mimi, Baba, naomba ya kwamba wataona ile nia, moyoni mwangu, na kusudi la Neno Lako ambalo ninajaribu kuwaletae, ya kwamba Mwokozi wao, Yesu, yuko pamoja nao. Yeye yu hai sikuzote, Yeye yu hai. Miaka elfu mbili ya ukosoaji na ubaridi haingemwua, Yeye angali hai papa hapa miongoni mwetu, usiku wa leo.

⁹⁵ Basi jalia watu wauone Uwepo Wake, wamwone akitenda kazi, sio kungojea mtu fulani kuwawekea mikono, lakini kwa imani wamwamini Kristo aliyefufuka, na kupokea uponyaji wao na wokovu wao. Waende huku na huku visiwani kila mahali, wakishuhudia kama maskini yule mama tuliyenena habari zake jana usiku, kwenye mji wa Sikari, na huko kwenye nchi ya Wasamaria. Tujalie, Bwana.

⁹⁶ Sisi ni watumishi Wako, tukijitolea kwa unyenyekevu pamoja na somo hili, usiku wa leo. Nena, Bwana, tuko mikononi Mwako, fanya nasi upendavyo. Katika Jina la Yesu tunaomba. Amina.

⁹⁷ Sasa, katika mikutano hii (kwa makasisi), nimejaribu kuiweka rahisi sana, ujumbe tu na... wa uponyaji, ili tuweze kumwangelia Bwana wetu. Sasa, mara nyingi watu huzunguka, mwajua, na ni binadamu tu, wanasema, "Loo, Ndugu *Nanii*, haleluya, hivi hufikiri alikuwa na karama ya Mungu? Aliniwekea mikono. Haleluya!"

⁹⁸ La, ni imani yako iliyofanya hivyo. Unaona? Ilikuwa imani yako, siyo mikono ya huyo ndugu. Ilikuwa ni imani yako, unaona, kwa sababu iwapo kuna uponyaji mikononi mwa mtu fulani, basi Kalvari ilipatwa na nini? Hapo ndipo *Yeye* alipolipia deni la uponyaji wetu. Ni imani yetu binafsi katika kazi Yake iliyokamilika. Mtu yeyote anajua hilo. Mnaona? Sasa, kwa hiyo, sikuja, kujaribu kusema, "Hebu sote tujitokeze na

hebu . . . tumwekee mikono.” Ninajaribu kusema haya ili kujenga imani yenu.

⁹⁹ Sasa, na mmoja wenu . . . Vipi kama mmoja wenu ndugu au dada wa Kihindi, angekuwa mgonjwa huku mbali katika mojawapo ya visiwa hivyo? Unawazia, “Vema, mimi ni maskini, sina pesa. Kama ningaliweza kwenda Marekani, nishuke huko mbali kwa Ndugu Branham, niende huko mbali mpaka kwa Oral Roberts. . .” Vema, labda Ndugu Roberts, labda ungechukua miezi kadhaa kuingia.

¹⁰⁰ Ninao mia tatu walioko mle kwenye orodha ya wanaongojea sasa, kutoka kote ulimwenguni, lakini hiyo ni kwa ajili ya mikutano ya faragha. Mnaona, tunapoingia mle, ninachukua kisa kama hicho, hatukiachi kamwe, tunaachana nacho mpaka Mungu atakapokifunua. Inamhitaji Mungu kufunua anachopaswa kufanya, yale amefanya, na kadhalika namna hiyo. Sasa, hayo ni mahojiano ya faragha, hilo ni jambo fulani maishani. Tunao huo mpango uliowekwa *hapa* katika Biblia, lakini maisha ya faragha ya vitu, loo, ingechukua miaka kadhaa, Ningeweza kuandika majuzuu ya vitabu juu ya yale nimemwona akifanya. Wala hakuna wakati mmoja liliwahi kushindwa. Hakuna hata wakati mmoja linaposhindwa. Mwulize tu mtu yeyote mahali popote, kamwe halishindwi. Haliwezi kushindwa, ni Mungu. Kuna jambo moja Mungu hawezi kufanya, hawezi kushindwa. Hawezi kushindwa.

¹⁰¹ Sasa, aminini sasa. Sasa, Yesu alikuwa akikemea kizazi hicho kwa kutokuamini ishara Yake aliyokuwa amewathibitishia ya kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Sasa, tulichukua hilo jana usiku, jinsi Yeye alivyokuwa Masihi kwa sababu alikuwa ni Neno. Je, hiyo ni kweli? Sasa, *Masihi* maana yake ni “Kristo, aliyetiwa mafuta.” Na ndipo alipaswa kuwa Mfalme, Nabii-Mungu, na huyu hapa alikuwa Roho ndani Yake. Sasa, kumbukeni wale ambao kweli walidumu na mafundisho ya Maandiko, walimtambua, lakini wale walioondoka na kanisa lingine katika mapokeo yao, walimkosa. Mnaona?

¹⁰² Naye Yesu akawaambia hao walimu, akasema, “Ninyi, pamoja na mapokeo yenu, mnazichukua amri za Mungu, na kuzitangua.” Sasa, wangepanya nini na mapokeo leo? Wakisema, “Siku za miujiza zimepita,” hayo ndiyo mapokeo yao; “Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu,” hayo ni mapokeo, sio Biblia. Ninaweza kumwonyesha mtu yeyote mahali ambapo Yesu alilitawaza Kanisa Lake na kuliagiza kwa “ulimwengu wote, kwa kila kiumbe. Na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa, nataka mtu fulani, anionyeshe sehemu fulani ya Maandiko ambapo Yeye aliliondoa kutoka kwa Kanisa, haipo. Bado liko Kanisani, ni mapokeo ndiyo yamelipotoshwa.

¹⁰³ Na hiyo ndiyo sababu hawakumtambua Yesu, kwa sababu mapokeo yao yalikuwa yamepotoshwa na kupata baadhi. . .

Walifikiri Masihi angekuja, na bila shaka walijenga hekalu, na kusema, “Atashuka kwenye ushoroba wa Mbinguni, watacheza bendi ya Malaika, Naye ataingia namna hiyo.” Naye alikuwa nini? Alizaliwa horini, katika ba—banda ambapo ng’ombe na wanyama walikuwa, katika sanduku dogo la majani, Naye alidhaniwa alizaliwa mwana haramu, mama Yake na babake hawakufunga ndoa. Wote... Loo, jamani. Ibilisi alichora pi—picha mbaya sana Kwake.

¹⁰⁴ Nao wakasema, “Mtu kama huyo? La. Alitoka shule gani? Elimu yake aliipata wapi? Mbona, baba yake alikuwa seremala, halafu aseme yeye ni Mwana wa Mungu.” Mnaona, wasingeweza kuamini jambo hilo. Lakini hata hivyo, Yeye alikuwa wa ajabu sana hata hawakuweza kukana kwamba lilikuwako, na ndipo wakasema tu, “Loo, yeye ni wa ibilisi.” Na hilo ni jambo lile lile siku hizi, wataliweka katika hali iyo hiyo, kwa maana hekima inajulikana kwamba ina haki kwa watoto wake.

¹⁰⁵ Hivi mlujua...? Kama nilivyotoa tamshi jana usiku, nilihisi ikienea juu ya kusanyiko, kwa namna fulani ilikuwa na hisia ya ajabu iliporejea, lakini niliposema, “Elimu imekuwa alama ya mpinga-Kristo kote katika nyakati.” Elimu ndiyo adui mbaya zaidi ambaye Injili imewahi kuwa naye. Sikilizeni, niko nje ya somo, lakini hebu kidogo tu. Hebu tuuchukue tu ule ukoo: Kulikuwa na Kaini na Sethi, Habili aliuawa ndipo Kaini akaletwa mahali pake, mauti, ufufuo wa Kristo. Nao watoto wa Kaini wote walikuwa werevu, wenye akili, wanasayansi, kote hadi siku za Nuhu. Nao watoto wa Sethi walikuwa wanyenyekevu, wakulima, wafugaji wa kondoo, wakulima wadogo kote kote. Na sikuzote imekuwa hivyo. Mnaona?

¹⁰⁶ Yesu alipokuja, Mafarisayo, na Masadukayo, na walimu, angalia walipokuwa. Wa kidini? Loo! Watakatifu? Jamani, usingeweza kutia kidole maishani mwao, lakini unaona, walikuwa wasioamini. Chochote kinachotilia shaka kituo kimoja cha Neno la Mungu ni mtu asiyeamini. Sijali wewe ni mtu wa kidini jinsi gani, Shetani ni wa kidini pia, huna budi kuliadini Neno. Na iwapo una Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu ataitikia kila Neno kwa... kila sentensi kwa “Amina.” Unaona? Hataondoa kamwe kutoka Kwake, ataliadini. Unaona?

¹⁰⁷ Kwa hiyo Yesu alipokuja, aliwapata wapi wanafunzi Wake? Je, Yeye alienda kwa Kayafa, sasa akasema, “Je, ni kundi gani lenye akili zaidi ulilo nalo?” Aliwapita hao, wasingemwamini. Alienda wapi? Alienda na kuwachukua Wahindi wa siku hizo, wavuvi kule mtoni, hiyo ni kweli kabisa, watu ambao hawangeweza hata kutia sahihi majina yao wenyewe. Biblia ilisema kwamba Petro na Yohana walikuwa wasio na elimu wala maarifa. Hiyo ni kweli. Lakini wangeweza kumponya mtu kwenye mlango ulioitwa Mzuri katika Jina la Yesu Kristo, na ilimpendeza Mungu kumpa mtu ambaye asingeweza kuandika

jina lake mwenyewe funguo za Ufalme, akisema, “Lolote utakalofunga duniani nitalifunga Mbinguni.”

¹⁰⁸ Kwa nini elimu ina sehemu kubwa hivi siku hizi, ikiwaondolea watu mbali na Mungu badala ya kuwaleta kwa Mungu? Paulo, unasema, “Vipi kuhusu Paulo?” Lakini Paulo alisema nini? Ilimbidi kusahau yote aliyowahi kujua, naye akasema, “Sikuja kwenu na hekima ya mwanadamu, kwa maneno makuu ya kuvutia, lakini...ili imani yenu ijengwe juu ya mambo kama hayo, lakini nilikuja kwenu katika nguvu za Roho, ili imani yenu iwe katika ufufuo wa Yesu Kristo.”

¹⁰⁹ [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...naye alikuwa akiwaambia, akiwakemea kwa sababu hawakumwamini, akasema, “Nisipozifanya kazi za Baba Yangu, basi msiniamini Mimi.” Naye huyu hapa akiwaambia.

¹¹⁰ Sasa, kumbukeni, Mungu, katika nyakati zote, daima amefanya mambo ya kimbinguni, kwa maana Yeye ni wa kimbinguni. Mliwahi kuwazia Mungu alikuwa nini? Hebu niwape picha ndogo tu sasa, kabla sijaenda. Loo. La, nitabarikiwa wala nisiweze kufanya hivyo. Naam, nitawapa, nitajaribu kwa vyovyote vile.

¹¹¹ Hapo mwanzo, kabla hapajakuwapo na chochote, ilikuwa ni Mungu. Kabla ya kuwako na kimondo, kabla hapajakuwa na nuru, kabla hapajakuwa na atomi, kabla hapajakuwa na molekuli, Yeye alikuwa Mungu. Lakini asingeweza...Alikuwa ni Nguvu kuu zinazotawala kila kitu. Naye alikuwa, kila kitu ndani Yake.

¹¹² Sasa, ndani Yake kulikuwa na sifa. Mnajua sifa ni nini? Inua mkono wako, mtu yeyote anayejua kile sifa...hakika mnajua sifa ni nini, kitu ambacho kiko, kiko ndani yako, ha—hakina budi kujionyesha chenyewe. Kama, sifa...Kama vile mnavyopenda mandhari, na mnapoona mandhari hiyo, kitu fulani, inaninii tu, loo, jamani, inakuchangamsha tu.

¹¹³ Sasa, katika Mungu, Yeye hakuwa Mungu bado, kwa sababu *Mungu* ni “Kitu cha kuabudiwa,” na hapakuwa na chochote cha kumwabudu, Yeye alikuwa Mungu, lakini hakuwa Mungu kwa namna hiyo. Halafu hapana shaka aliwaumba Malaika, ndipo wakaanza kumwabudu. Kisha, Yeye alikuwa na sifa za kuwa Baba; jambo lingine, Yeye alikuwa na sifa za kuwa—kuwa Mwana; jambo lingine, alikuwa na sifa za kuwa Mponyaji; jambo lingine, sifa za kuwa Mwokozi. Mnaona? Nayo mambo haya yote yalipaswa kujionyesha. Mnaona? Naye Mungu, ati amfanye mwanadamu kutenda dhambi, ili aweze kumwadhibu? La. Basi alimweka juu ya msingi wa uhuru wa kujichagulia, naye mwanadamu akatenda dhambi mwenyewe, na kwa hiyo basi Mungu akawa Mwokozi basi. Mnaona?

¹¹⁴ Kwa hiyo tunazooni ni sifa tu za Mungu zikijidhihirisha zenyewe, na kila kitu kiko kwa wakati wake kikamilifu, kila

karama, kila kitu kinakwenda sawasawa kabisa na mpigo wa saa, mnaona, yuko pale pale.

¹¹⁵ Sasa, Yesu katika wakati Wake, Yeye alikuja kuonyesha sifa za Mungu, ndani Yake Mungu alidhihirishwa ndani Yake. Angalieni. Sasa, Yeye alikuwa ameonyesha ishara hii ya Kimasihi. Ilikuwa ni kutokuamini. Naye Mungu katika nyakati zote amekuwa na ishara kwa watu, na sasa, watu walipoamini ishara hiyo, ulikuwa ni wakati wa ufanisi mkuu kwa watu, lakini waliposhindwa kuamini, ikawa ni machafuko kwa watu. Hakika. Sasa, hebu ninukuu hilo tena, maana nitachukua dakika chache tu sasa.

¹¹⁶ Angalieni, Mungu anapotuma karama, nao watu wakaiamini, ni wakati wa utukufu kwa hao watu, lakini Mungu anapotuma karama, nao watu wanaikataa, kizazi hicho kinaingia kwenye uharibifu. Sasa, angalieni. Vipi kama ulimwengu leo hii ungeipokea karama ya Mungu?

¹¹⁷ Hebu turudi nyuma kwa dakika moja. Nuhu alikuwa... alikuja na karama ya Mungu kama nabii, akisema kunakuja dhoruba ambayo ingeifunika dunia nzima kwa maji. Sasa, haikuendana na mawazo ya kisayansi ya siku hiyo. Kumbukeni, walikuwa wanasayansi wakubwa wakati huo kuliko tulivyo sasa, walikuwa wamejenga piramidi na Sfiniksi, wala tusingeweza kuijenga hiyo sasa. Waliupaka mwili dawa kuufanya uonekane wa kawaida, hata wa leo, mumiani, tusingeweza kuufanya. Walikuwa na rangi ambazo tusingeweza kugusa, walikuwa wanasayansi wakubwa kuliko tulio nao siku hizi. Na sasa, wakati... Pengine wangeweza kurusha rada mwezini, pia.

¹¹⁸ Naye Nuhu, mtu huyu aliyesimama kule nje, baada ya kusikia kutoka kwa Mungu, na kuhubiri, akitabiri kwamba Mungu angeuangamiza ulimwengu kwa maji, "Mvua itanyesha kutoka mbinguni."

¹¹⁹ Mbona, ninawasikia wanasayansi wakija kule, na kusema, "Angalieni, tuna chombo ambacho tunaweza kukirusha hadi mwezini." Mnajua, kamwe haikuwa imenyeshwa katika siku hizo, Mungu aliinyesha dunia kutoka kwenye chemchemi, hakukupata kuwa na mvua angani. Dunia, ikiegemea nyuma baada ya yale maangamizi yaliyotangulia ile gharika, husababisha mvua. Kwa hiyo Nuhu akasema kwamba itanyesha kutoka juu, nao hao watu hawakuamini, sayansi inasema, "Hakuna hata tone moja la mvua huko juu, hakuna maji. Ingewezaje kunyesha?"

¹²⁰ Nuhu angesema, "Kama Mungu alisema itanyesha, na mvua inakuja kutoka huko juu, Mungu ana uwezo wa kuweka mvua huko juu." Mnaona? Lakini hao watu hawakuamini. Siku moja ikanyesha. Mnaona? Na jamii hiyo, kwa sababu hawakuamini, waliangamizwa, ulimwengu mzima.

¹²¹ Miaka mingi baadaye, akaja nabii, aliyeitwa Musa, akashuka kutoka nyikani, Nguzo ya Moto juu yake. Naye alikuwa akiwaletea ahadi ya Mungu, akiwaambia ya kwamba Mungu alikuwa ameahidi, kwa Neno Lake, kuwapeleka kwenye nchi iliyojaa maziwa na asali. Naye alikuwa na hii Nguzo ya Moto juu yake, naye Mungu alikuwa akifanya kazi pamoja naye kuwathibitishia hao Wayahudi ya kwamba yeye alikuwa nabii.

Akasema, “Kesho, tayarisheni kila kitu, kwa sababu jambo *fulani-fulani* litatendeka.” Nalo likatendeka sawa kabisa, yeye alikuwa nabii.

¹²² Angalieni. Niliwazia, hivi majuzi, jinsi jambo hilo halina budi lilikuwa tukufu kwa Israeli waliposikia hivyo. Walimwamini. Angalieni, walikuwa—walikuwa watumwa. Wao—wao—wanawatupia mkate uliooza, wakaula, la sivyo walikosa. Kama hao Wamisri wanataka kuwachukua binti zao na kuwabaka, wangepanya nini juu yake? Hakuna. Waende na kuwachukua wanao wachanga, na kuwaua, wangeweza kufanya nini kuhusu hilo? Hakuna. Walikuwa watumwa, na hata hivyo walikuwa watu wa Mungu. Amina.

¹²³ Angalieni. Sasa, hawa hapa, watu wa Mungu katika hali ya namna hiyo, basi akashuka nabii huyu akiwa na BWANA ASEMA HIVI, kulingana na Maandiko, “Mungu, Baba zetu walikutana na Ibrahimu na kumwambia ya kwamba uzao wake utakaa katika nchi ya kigeni kwa muda wa miaka mia nne, kisha atawatoa kwa ahadi kubwa na uwezo. Angewakombo, na kuwapeleka kwenye nchi nzuri ambayo Ibrahimu alikaa, nayo . . . wakati huo umekaribia.”

¹²⁴ Mtu yeyote angaliweza kusema hivyo, lakini mtu huyu alikuwa na Nguzo ya Moto juu yake, naye alikuwa nabii, alichokuwa akisema kilikuwa kikitendeka jinsi alivyosema. Loo, jamani!

¹²⁵ Israeli waliamini jambo hilo. Walifanya nini? Walitoka Misri taratibu, chini ya ile Nguzo ya Moto, wakienda zao kwenye nchi ya ahadi ambayo hawakuwahi kuiona wala kujua lolote kuihusu. Wala hakuna hata mmoja wao aliyepata kuwa kule, bali walikwenda kwa sababu Neno la Mungu liliwaamuru waende, walikuwa kwenye wajibu wao.

Natumai sipigi kelele sana. Nimezoea kuhubiri nje na kadhalika. Hebu kidogo. Angalieni. Nitasimama nyuma kidogo.

¹²⁶ Angalieni, walimfuata nabii huyo nyikani, naye Mungu akawalisha nyikani, alikidhi mahitaji yao yote, akanyesha mkate kutoka mbinguni wakati wa usiku na kuwalisha, kisha akawapandisha mpaka mahali paitwapo Kadesh-barnea. Kadesh-barnea ilikuwa, wakati mmoja, kiti cha hukumu cha ulimwengu.

¹²⁷ Nao walikuwa na shujaa mkuu pamoja nao aliyeitwa Yoshua. Nalo neno *Yoshua* linamaanisha “Yehova-Mwokozi.” Alitoka

nje ya kambi, akavuka Yordani, hakuna mtu ambaye hajawahi kufika huko sasa, hawakujua hiyo nchi ilikuwako, ila tu kwa ahadi ya Mungu, naye akavuka Yordani, akaingia kwenye nchi ya ahadi, na kuleta ushahidi ya kwamba hiyo nchi ilikuwa vile vile tu Mungu alivyosema. Mnaona? Ilikuwepo.

¹²⁸ Na ilikuwa ni wakati huo ambapo watu, asilimia tisini yao, hawakumwamini Yoshua, iliwabidi kutangatanga kwa muda, lakini Mungu, akitoa ahadi, aliwavusha. Jinsi linavyopendeza. Haikuwabidi kufanya kazi chini ya Farao, wangeweza kuoa wake zao, kuwajengea nyumba ndogo mahali hapo, walime chakula chao wenyewe na kadhalika, na kukila, na kuwalea watoto wao kwa amani. Mataifa yaliwaogopa na kadhalika. Ndipo baada ya muda kidogo vilima vya nchi hiyo nzuri vilijaa makaburi.

¹²⁹ Kisha akaja Shujaa mkuu kuliko wote, Yesu. Naye akasema Mungu ameandaa Mahali pasipo na mauti, amina, ambapo tunaweza kuishi milele, kujenga nyumba na kukaa ndani yake, kupanda mizabibu, na kula matunda yake, wala hatutayaachia mtu mwingine. Amina. “Nyumbani mwa Baba Yangu mna makao mengi. Kama sivyo, ningeliwaambia. Nami naenda kuwaandalia mahali, kisha nirudi tena kuwapokea Kwangu, ili nilipo Mimi nanyi muwepo.” Aliahidi hilo, ya kwamba kuna Uzima baada ya mauti. Yoshua mwingine mkuu, hakuna mtu aliyewahi kwenda kule, na karudi, Yoshua mwingine mkuu tu.

¹³⁰ Angalieni. Ndipo alipofika mahali hapo, alikutana na Kadesh-barnea Yake, kiti cha hukumu kwa ajili yetu sisi sote, Kalvari. Hapo ndipo alipohukumikiwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu. Alivuka Yordani ya mauti, tunaogua, akaingia katika hiyo nchi nyingine, akafa. Alikufa kabisa hata jua likaacha kuangaza, mwezi usingeangaza, na mbona, dunia ilishikwa na baridi ya wasiwasi wakati miamba ilipotikisika kutoka kwayo, hapo alipokufa. Naye akafa, lakini siku ya tatu akarudi kutoka ng'ambo ya Yordani, akirudi na ushahidi ya kwamba mwanadamu huishi baada ya kufa hapa. Ni Shujaa mkubwa jinsi gani!

¹³¹ Sasa, Yeye alisema, “Nitawapa arabuni ya wokovu wenu.” Mnajua arabuni ni nini? Ni malipo ya kwanza. Ni kama ikiwa ningetaka kununua mashua kutoka kwa mmoja wenu ninyi ndugu wa Kihindi, nikatoka nje na kusema, “Unataka ngapi kwa mashua hiyo?”

Useme, “Dola elfu mbili.”

¹³² Niseme, “Vema, nitakwambia ninalofanya, nitakupa dola hamsini ili uishikilie hadi wiki ijayo. Je, utafanya hivyo? Unishikilie. . . Je, utaishikilia kwa ajili yangu?”

¹³³ “Nitafanya hivyo, Ndugu Branham.” Halafu unipe risiti, nami nikupe dola hamsini. Sasa, huwezi kuiuza mashua hiyo,

kwa sababu nilipata zabuni yake ya kwanza. Hiyo ni arabuni kwamba nitaipata hiyo mashua, ni mali yangu.

¹³⁴ Vema sasa, Mungu alirudi, na kusema, “Pandeni mwende huko Yerusalemu, mkangoje. Nitawatumia Arabuni ya wokovu wenu.” Nao walikuwa huko juu wote kwa moyo mmoja mahali pamoja, ndipo ghafla ikaja ile Arabuni, ikashuka kutoka Mbinguni kama upepo wa nguvu ukienda kasi, na kuijaza nyumba yote walimokuwa wameketi.

¹³⁵ Sasa, angalieni hapa, tunaweza kuangalia nyuma na kuona ambapo tulikuwa wasioamini wakati mmoja. Tumeona wakati mmoja ambapo tuliukaribia mkutano kama huu na kuucheka. Tuliona wakati mmoja, huko nyuma maishani mwetu, ambapo tungekosoa uponyaji wa Kiungu. Sisi, wakati mmoja hatukumwamini Mungu, wakati mmoja hatukuamini Neno Lake. Lakini sasa tumefufuliwa kutoka huko, tumeinuliwa juu, tukafa katika Kristo, tukazikwa pamoja Naye, tukafufuliwa pamoja Naye katika ufufuo Wake, na sasa tumeketi katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu. Wakati mmoja. . .

¹³⁶ Mnaona, Arabuni. . . Sisi hapa, leo hii, katika Arabuni ya wokovu wetu. Tumesimama hapa, usiku wa leo, tumekufa tayari, tukazikwa katika Kristo, na kufufuliwa pamoja Naye, na tumeketi katika mahali pa Mbinguni, tukifurahia mambo ya kiroho tukirudi kutoka ng’ambo. Mnaona, mahali pa Mbinguni. Loo jamani, inatufanya tupaze sauti kuwazia juu yake.

¹³⁷ Kama vile maskini yule mwanamke mweusi, mwanamke Mnegro, dada, alivyosema huko Marekani, alisema, “Dk. Branham,” kasema, “Mimi—mimi nataka kutoa ushuhuda.”

“Endelea, Dada, shuhudia.”

¹³⁸ Akasema, “Ninataka kusema hivi, enyi watu: Siiko,” Hilo ni neno wanalotumia kusini. Kasema, “Siiko kile ninachopaswa kuwa, wala siiko ninachotaka kuwa, lakini basi, jambo lingine nijualo, siiko nilivyokuwa.” Hilo ni jema. Alijua jambo fulani lilikuwa limetukia. Amina. Vivyo hivyo na mimi, kila mtu aliyezaliwa na Roho wa Mungu anajua wewe si vile ulivyokuwa. Amina. Mimi si kile ninachotaka kuwa, wala si kile ninachopaswa kuwa, wala si kile nilichokuwa. Mnaona? Nimefufuka pamoja Naye. Sasa, niko juu *hivi*, nikingojea kubadilishwa kwangu kuje.

¹³⁹ Sasa, Musa, Musa alikuwa mtumishi wa Mungu. Sasa, Yesu akizungumza hapa, Yeye alisema, “Watu wa Ninawi watasimama katika hukumu kwa sababu walitubu kwa mahubiri ya Yona.” Yona alikuwa nabii.

¹⁴⁰ Sasa, watu wengi humsema tu vibaya maskini mzee Yona, nao walisema alikuwa m—mtu aliyerudi nyuma. Sidhani hivyo. Nafikiri Biblia ilisema kwamba hatua za wenye haki huamriwa na Bwana. Sasa, tunafanya mambo ambayo hayaninii. . . hatuelewi kwa nini tunayafanya, lakini tunanyamaza tu kimya,

maadamu tunaongozwa na Roho, tunaenda kuyafanya kwa vyovyote vile. Yanaweza kuwa ni kinyume na mawazo yetu, lakini wakati Roho Mtakatifu akisema, “Nenda,” tunaenda.

¹⁴¹ Kwa mfano, sasa hivi nina mkutano, utakaofanyika New York, sina budi kuufanya juma hili, ambapo kulikuwa na watu mia tatu wanaozungumza Kihispania waliochukua Bustani ya Madison Square inayotoshea watu elfu kumi na tisa, na nilitaka juma lili hili, hapa, ambalo niko humu, niwe huko New York. Mnaona? Lakini Roho Mtakatifu aliniongoza hapa, inaonekana kana kwamba ingekuwa kinyume, lakini sijui ni kwa nini, bali niko hapa. Mnaona, “Watoto wa Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu.” Hatuelewi. Mnaona?

¹⁴² Sasa, hao ndugu wengine wanaweza kuwaendea hao watu. Sasa, kama vile Ndugu Roberts, asingeweza kwenda kule, asingeweza kuja hapa, inambidi kuwa na karibu, nafikiri, ni karibu dola elfu kumi na tano hadi ishirini kila siku, vipindi vya televisheni, na mambo ya kila namna, na—na jengo la dola milioni tatu huko kufanyia kazi. Ndugu huyo hangeweza kuja hapa, msingeweza kuunga mkono kitu kama hicho, ninyi sio. . . hamwezi kumudu kufanya hivyo. Mnaona? Na wala Tommy na mpango wake mkuu, pamoja na maelfu ya wamishenari kote nchini, asingeweza kufanya hivyo.

¹⁴³ Kwa hiyo mnaona, Bwana hakuniacha nipanuke hivyo, aliniacha tu nibaki hivi nipate kuingia kwenye kona yoyote ndogo, maana sihitaji kitu ila Uwepo Wake tu. Hiyo ni kweli. Nilikuwa hudumani kabla ya ndugu yeyote kati ya hao. Lakini mnaona, Bwana amenena nami, akisema, “Usichukue chochote cha hayo, usijichanganyishe na pesa, achana nazo.”

¹⁴⁴ Sikuwahi kuchukua sadaka maishani mwangu mwote. Nimekuwa nikihubiri kwa miaka thelathini na mmoja na kamwe sikuchukua sadaka maishani mwangu. Mnaona? Kwa sababu. . . Na ninashikilia ninii. . . Nilifanya mikutano ya watu wapatao laki tano katika kusanyiko moja, kisha nikaenda na kufanya mkutano ambapo kanisa huketi watu ishirini tu, lakini Bwana alisema, “Nenda.” Mnaona? Popote pale asemapo, “Nenda,” nenda.

¹⁴⁵ Hapa si muda mrefu uliopita. . . Mmesikia juu ya Ndugu Roberts, mtu mashuhuri. Nami nikaenda. . . Loo, yeye ni ndugu mzuri sana, rafiki msiri wangu, nami nikaenda kwenye jengo lake kubwa mno. Nikaenda kwa Tommy. Naye Tommy alikuwa hapa chini Po—Portland wakati yule mwendawazimu alipojitokeza kunia usiku huo, jukwaani, mmeisikia hiyo hadithi, jamaa mkubwa mno, na kasema, “Nitakupiga nikurushe huko, katikati ya kusanyiko lile. Nitavunja shingo yako.”

Ndipo Roho Mtakatifu akasema, “Kwa sababu umelisahi Neno la Mungu, utaanguka miguuni pangu.”

kasema, “Nitakuonyesha ni miguu ya nani nitakayoangukia,” akavuta ngumi yake kubwa.

Nami nikasema, “Toka ndani yake, Shetani,” naye akaanguka kuingama miguu yangu, sawa kabisa, huyo hapo.

Kwa hiyo Tommy alikuwa amesimama pale. Polisi wakaja mbio na kusema, “Tunamtafuta mtu huyo tupate kumweka gerezeni.” Kasema, “Kwani amekufa?”

¹⁴⁶ Nikasema, “La, bwana, lakini mfingirisheni atoke miguuni mwangu.” Mnaona? Alikuwa na uzito wa kama—kama mia mbili na hamsini, kwa hiyo wakamfingirisha kutoka miguuni mwangu, naye huyo hapo.

Akasema, “Je, ameponywa?”

¹⁴⁷ Nikasema, “La, bwana, yeye anaiabudu hiyo roho. Hataweza...” Nilikuwa nimewaongoza maskini hao polisi wawili kwa Kristo kwenye chumba cha kubadilishia nguo, kule nyuma, kwenye... kwenye Ukumbi wa Portland.

¹⁴⁸ Sasa, sasa, mnaona, katika hilo Tommy akawa mtumishi wa Mungu, na sasa yeye... na akienda huko nje hudumani, amefanya kazi kubwa. Naye Ndugu Oral, hilo hapo jengo lake kuu. Vema, ni jambo zuri sana kuwazia kuwa mtu mmoja, mtu mmoja angeweza kujenga jengo la dola milioni mbili na nusu au tatu. Whiu, jamani! Kisha angalia To-...

¹⁴⁹ Nilikwenda kwa Oral, na kuna mashine mia tano za IBM zinazofanya kazi, barua zake hazigusi mikono ya wanadamu, kuna mashine inayozikota, inaziandika, inazishusha, ikazikunja, na kuzituma. Anaenda kwenye benki, anachukua pesa, na kuzileta ndani kwa lori kubwa mno, na kuzitupa kwenye ninii... Kichukuzi huzunguka katika lugha mbalimbali, wanavivuta nje, namna *hiyo*, na wanazitunza hizo pesa. Mbona, ni ninii... Hujawahi kuona kitu kama hicho maishani mwako. Na ni jambo kubwa. Naye Oral akiniongoza apate kunionyesha, Ndugu Fisher, yule anayefanya umishenari pamoja naye kule.

Ndipo basi nilikuwa nimeliona la Ndugu Tommy, mahali pake pakubwa kule, nikawazia, “Jinsi lilivyo zuri, jinsi linavyopendeza.” Ndipo ikatokea niliangalia nje. Ndugu...

¹⁵⁰ Hao polisi walikuja, kasema, “Ndugu Branham, huwezi kutoka nje ya mlango huo.” Kasema, “Kuna watu hamsini wamesimama huko nje wakikungoja.” Kasema, “Wangeninii... Wanangojea tu kuona...”

Nami nikasema, “Vema, kuna mlango wa nyuma?”

Kasema, “Naam, toka nje kwa kupitia *hapa*.” Sasa, nao wakasema, “Tutamtuma mtu huko kukuchukua.”

¹⁵¹ Nami nikatoka nje kwenye sehemu ya nyuma ya kuegeshea magari. Nami nilikuwa nikitembea huku na huko kule chini nikilitazama jengo hilo kubwa. Loo, jamani, kama tu... Sijapata

kuona kitu chochote, katika sehemu yoyote ya ulimwengu, kama hicho; mvulana mdogo wa Kipentekoste alifanya hivyo.

¹⁵² Nikawazia, “Si ajabu hiyo?” Nikawazia, “Mungu, ni ajabu jinsi gani!” Kisha nikawazia, “Wazia tu juu ya mahali pa Ndugu Tommy kule, jinsi ambavyo jengo hilo kubwa mno, karibu bloku moja ya jiji, katika kuchapisha tu vitabu, na makatibu, na kadhalika, na mitambo ya IBM inayofanya kazi.”

¹⁵³ Nikawazia “Jamani, ningechukia wao kuja kwangu kuangalia pangu.” Nina taipureta moja ndogo iliyowekwa mwishoni mwa trela, wala nisingeninii... kujaribu kumtafuta mtu wa kunisaidia kujibu barua zangu.

¹⁵⁴ Nami nikawazia, “Lakini jamani, nisingekuwa na jukumu hilo lote bure, sina akili za kutosha kushughulikia hayo.” Nikawazia, “Mungu alijua hilo.”

¹⁵⁵ Nami nilikuwa nimesimama pale, ndipo nikawa na moyo mzito kweli. Nikaanza kuwazia, “Mungu, kila mmoja wa hawa ndugu alisema kwamba waliona huduma Wewe uliyonipa, nayo ikawafanya waingie hudumani,” nikasema, “kwa jambo hilo, nashukuru, sote tunafanya kazi kwa ajili ya Mahali pamoja pakubwa, huko juu, panapoitwa Mbinguni.” Nami nikasema, “Ninashukuru kwa hilo.” Lakini nikasema, “Nadhani labda usingeweza kuniaminia, Nawe ulijua nisingeweza, kuchukua pesa namna hii, wala nisingekuwa na akili ya kujua la kufanya nazo kama ningezichukua.” Nami nikasema, “Nadhani ilitokea tu kuwa hivyo.”

¹⁵⁶ Sasa, nilikuwa nimesimama hapo, kwa namna fulani nikajisikia kusongwa kidogo kooni mwangu, kwa sababu... Sasa, sisemi hivi... Ninasema tu hili, ukweli. Nikasikia Sauti dhahiri tu kama vile mnavyonisikia, ikasema, “Lakini Mimi ndimi Urithi wako.”...?...

¹⁵⁷ Nikasema, “Asante, Bwana, nitaenda popote, mahali popote, wakati wowote. Nataka kufanya yale Wewe—yale Wewe ungetaka nifanye,” na kumshukuru Mungu. Sasa, Ndugu Osborn, na Ndugu Roberts, na Ndugu...hao ndugu wote wa thamani kote duniani, sote tunafanya kazi kwa ajili ya Mahali pamoja, Mahali pamoja. Mnaona?

¹⁵⁸ Nayo hii, karama ndogo ambayo Bwana alinipa, ni ya kupenya kwenye kona hizi ndogo. Huwezi kufungwa kabisa na pesa, na ratiba, na mambo kama hayo. Penya tu kwenye kona hizi ndogo na kulianzisha jambo hilo, hivyo tu. Nami ni—ni—ninashukuru kwa ajili ya sehemu hii. Na nina furaha sana; Yeye ndiye Urithi wangu, na Yeye ndiye ninayemngojea.

¹⁵⁹ Sasa, Yona alikuwa na tiketi ya kushuka kule, naye alitaka kwenda Ninawi, kile ambacho Mungu alimwitia kufanya, lakini akaenda Tarshishi. Sasa, unawazia, “Vema, alifanya vile hasa Mungu alimwambia asifanye.” Lakini hebu kidogo, kama nabii anaongozwa na Bwana, daima hutokea kuwa

sahihi. Sasa, alitoka kule nayo dhoruba ikatokea, na—nayo bahari ikachafuka, nayo hiyo mashua ilikuwa ikizama, nao wakamfunga Yona mikono na miguu yake, na kumtupa baharini, ndipo nyangumi akammeza.

¹⁶⁰ Sasa, si muda mrefu uliopita, walikuwa na nyangumi amelazwa kwenye m—mkokoteni mkubwa huko Louisville, Kentucky, yapata miaka kumi na mitano iliyopita, ama labda ishirini. Nao walikuwa wakitoa hotuba, naye maskini yule mwanasayansi aliyekuwa akitoa hotuba alikuwa akiidhihaki Biblia. Hivi ndivyo alivyosema, alisema, “Sasa, ninawataka ninyi watu, mnajua ile hekaya...” Ati hekaya? Biblia hii si hekaya, ni Kweli. Naye akasema, “Ile hekaya kuhusu ati nyangumi kammeza Yona,” akasema, “Nawatakeni muone, usingeweza kuchukua besiboli ya ukubwa mzuri na kuiweka kwenye koo la nyangumi huyo. Basi kwa mujibu wa hekaya hiyo, haina maana. Huyu ni nya—nyangumi mzuri, wa kawaida, wala nyangumi asingeweza kummeza mtu, kwa sababu hangeweza kupita kooni mwake. Ni...Ni... Kadiri unavyoweza kuinyoosha itakuwa karibu inchi nne tu, ambazo huyo mtu asingeweza kupitia, wala asingaliweza kufanya hivyo.”

Hilo liliizidia sana asili yangu ya Kiairishi, mwajua, nikasema, “Bwana, nataka kusema neno.”

Akasema, “Naam, bwana. Ni nini?”

¹⁶¹ Nikasema, “Kamwe hujui Biblia yako.” Nikasema, “Mungu alisema ya kwamba alimweka tayari samaki huyu, huyu alikuwa ni *ndege* aliyejengwa maalum. Mnaona? Mungu alimtayarisha samaki huyu, alikuwa wa aina tofauti.”

¹⁶² Huyu—huyu, a—angeweza...a—angeweza kumeza nyumba kama angetaka. Mungu anaweza kufanya atakacho. Biblia ilisema Mungu alimweka tayari samaki. Loo, alikuwa na koo kubwa ndani yake. Mnaona?

¹⁶³ Na hivyo Yona akaingia tumboni mwa yule samaki. Nanyi kina mama mnajua sasa, mnapomlisha samaki wenu mdogo wa dhahabu, mnajua anachofanya? Anashuka moja kwa moja hadi chini kabisa ya maskini beseni hiyo, na kuweka pezi zake ndogo chini, na kupumzika. Ameshiba kabisa. Mnaona? Amelala humo akipumzika tu. Amekwisha kuzungukazunguka majini mpaka akapata chakula chake, kisha akashuka na kupumzika. Hivyo ndivyo samaki wafanyavyo, wanapokula, wanaposhiba kabisa, wanarudi. Samaki wa maji safi hapa wataingia chini ya mwamba mahali fulani na kupumzika. Hiyo ndiyo njia. Nami nawazia maskini samaki huyu mkubwa alishiba mlo wa nabii huyu. Kwa hiyo anashuka majini, na kwenda chini kabisa, na kulala.

¹⁶⁴ Sasa, nena kuhusu Yona kuwa katika hali fulani! Alikuwa katika hali mbaya. Watu wengi huzungumza juu ya dalili, wanasema, “Vema, niliombewa jana usiku, lakini uhum, ningali

naumwa.” Hilo halina uhusiano wowote nalo. “Niliombewa, mkono wangu ungali umelemaa.” Hilo halina uhusiano wowote nalo. Kama unaamini, huangalii huo, unaangalia ahadi. Unaona? Huuangalii huo mkono, hizo ndizo tunazoita dalili, kuangalia dalili.

¹⁶⁵ Sasa, hakuna mtu hapa ndani angeweza kuwa na dalili kama Yona. Ndugu, alikuwa na kisa kibaya zaidi cha dalili nilichowahi kuona. Angalieni hapa. Kila...Sasa, alikuwa—alikuwa huko nje baharini, mikono na miguu yake imefungwa nyuma yake, naye alikuwa ndani ya tumbo la nyangumi, pengine mita kadhaa kwenda chini, amelalia matapiko katika tumbo la nyangumi katika bahari yenye tufani. Sasa, nena kuhusu dalili! Akaangalia *huku*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi, *huko*, ilikuwa ni tumbo la nyangumi. Kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi. Hakuna mtu aliye katika hali mbaya kama hiyo hapa. Angalieni vile...Angalieni dalili alizokuwa nazo.

¹⁶⁶ Lakini mnajua alichosema? Alisema, “Ni ubatili wa uongo. Sitaamini hata moja.” Akasema, “Bwana,” akapinduka mgongoni mwake, amezungukwa na matapiko pande zote, mwani umeizinga shingo yake, akasema, “mara nyingine tena nitatazama kukabili hekalu Lako takatifu.” Loo! Sio, “kutazama tumbo la nyangumi,” au hali ya mambo, lakini, “kutazama hekalu Lako takatifu.”

¹⁶⁷ Sulemani, wakati Sulemani alipoweka wakfu hekalu hilo aliomba, akasema, “Bwana, ikiwa watu Wako wana shida wakati wowote, na kukabili mahali hapa patakatifu, basi usikie kutoka Mbinguni.” Basi Yona akatenda kulingana na maombi ya Sulemani. Ndipo Mungu, sijui alichofanya, aliweka hema la oksijeni huko chini ama chochote kile, na akamweka hai siku tatu mchana na usiku.

¹⁶⁸ Sasa, hatuninii...Hatuko katika hali hiyo mbaya, hakuna hata mmoja wetu aliye katika hali mbaya kama Yona alivyokuwa. Hiyo ni kweli, kwa maana huyu hapa Roho Mtakatifu hapa. Hatuko katika tumbo la nyangumi, ha—hatuko katika hali hiyo. Lakini kama Yona, chini ya mazingira hayo, angeweza kutazama hekalu ambalo mwanadamu aliliombea alipoliweka wakfu, huku huyo mtu aliyeliombea alirudi nyuma baadaye, na Mungu akayasikia maombi yake, ni zaidi sana vipi chini ya hali hii ya mambo tunaweza kutazama Mbinguni, ambapo Yesu ameketi mkono wa kuume wa Mungu, akiishi daima kufanya maombezi tunapoungama? Jamani, jamani! “Sitaangalia maumivu ya tumbo langu. Sitaangalia moyo wangu, unaopiga vibaya. Sitaangalia mkono wangu uliolemaa. Lakini nitatazama kwenye ile ahadi, kwa kuwa Yeye ameketi pale yu hai sikuzote ili kufanya maombezi.” Amina.

¹⁶⁹ Ninataka kuwaonyesha jambo fulani sasa, niwaonyeshe ambapo Mungu anajua anachozungumzia. Sasa, watu wa

Ninawi, hilo lilikuwa jiji kubwa, yapata watu nusu milioni, karibu sana na ukubwa wa St. Louis, Missouri, nao walikuwa makafiri, walikuwa katika dhambi ya kila namna. Waliabudu wanyama, na sanamu, na kila kitu, nao walikuwa...kazi yao walikuwa wavuvi. Na kwa hiyo nyangumi alikuwa mungu wa bahari.

¹⁷⁰ Kwa hiyo wote walikuwa wametoka yapata saa tano wakivua samaki, wavuvi wote wakivuta nyavu zao huko nje, baharini, ndipo muda si muda mwajua, akaja mungu wa baharini, nyangumi, akakimbilia ukingoni, akauchomoa ulimi wake, naye nabii akatokea akitembea moja kwa moja ukingoni. Hakika walitubu. Mungu alijua la kufanya. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo kwa watu wanaotaka kuamini. Mnaona?

¹⁷¹ Yona hakuwa nje ya mapenzi ya Mungu. Mnaona, yule mungu nyangumi alitema nabii moja kwa moja ukingoni, hakika wataamini Ujumbe wake. Basi huyo hapo akatokea.

¹⁷² Naye Yesu alisema ya kwamba, mwajua, ya kwamba kulikuwako na aliye mkuu kuliko Yona pale. Lakini angalieni alichosema. Sasa, kidogo kabla hatujaliendea somo lingine. Angalieni. Yesu alisema...Walisema, “Mwalimu, tutaona ishara.” Vifungu vitatu nyuma ya pale nilipoanzia kusoma. “Bwana, twataka kuona ishara.”

¹⁷³ Akasema, “Kizazi kibaya na cha zinaa chatafuta ishara.” Je, hiyo ni kweli? Naye akasema, “Hakuna ishara itakayopewa kizazi hicho,” sasa, sikilizeni, kwa makini. Ni wangapi wanaojua ya kwamba—ya kwamba Maandiko hujirudia Yenyewe daima? Tunajua hilo. Naye akasema, “Hakuna ishara itakayopewa kizazi hicho kibaya, kiovu, cha zinaa,” hicho ni kizazi hiki.

¹⁷⁴ Hakujawahi kuwa na uovu mwingi na uzinzi, ulimwenguni kote, kama ulivyo sasa hivi, upotovu. Vema, mashoga, upotovu, wanawake mitaani, wamevua nguo, kila...Wewe...Ni vibaya sana jinsi watu wanavyofanya ulimwenguni kote, na hasa katika—katika Marekani. Na inakaribia kuwa mbaya vivyo hivyo nchini Canada, ni mbaya mno, lakini ni kweli. Taifa hilo kubwa, taifa hili dogo ni mfano wake, msichukue kielelezo chenu kutoka kwao, chukueni kielelezo chenu kutoka *Hapa juu, Kristo*.

¹⁷⁵ Angalieni. Basi hao hapo, waovu...Yeye alisema, “Hakutakuwa na...” Sasa, sikilizeni, kwa makini, msije mkalikosa. “Watapokea ishara. Kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, hivyo ndivyo Mwana wa Adamu atakavyokuwa katika moyo wa nchi siku tatu mchana na usiku.” Watapokea ishara hiyo. Ni nini...? Ishara ya ufufuo. Mnalipata? Hiyo ndiyo hasa tunayopata sasa, ishara ya kwamba Yeye hajafa, Amefufuka katika wafu na yuko miongoni mwetu, akifanya mambo yale yale aliyofanya

alipokuwa hapa duniani. Nacho kizazi kibaya na cha zinaa, mnaona, kingepokea ishara hiyo.

¹⁷⁶ Kisha, moja zaidi, tunafunga. Yeye alisema, “Naye malkia wa kusini atasimama siku ya hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu. kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na tazama hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.”

¹⁷⁷ Sasa sikilizeni, katika kufunga. Katika kizazi cha Sulemani, Mungu alitoa karama kwa nchi, na hiyo ilikuwa ni karama ya upambanuzi, nayo ikamwangukia Sulemani, ndipo watu wote wakaiamini kwa moyo mmoja. Vipi kama watu wote leo hii wangeamini? Vipi kama Canada, na Marekani wangeamini Karama yao ambayo Mungu aliwatumia, Roho Mtakatifu? Vipi kama watu wote waliodai kuwa Wakristo wangeliamini tu Hiyo? Mbona, haingetubidi kuwa na wasiwasi kuhusu mabomu ya atomiki ya Urusi na mambo hayo yote.

¹⁷⁸ Naam, sisi... Hutaweza kamwe kuchimba nje ya njia ya bomu la atomiki. Vema, hilo jambo... Watu wanachimba mashimo, na huko Marekani wanashuka kwenye mapango na kutengeneza ofisi za serikali. Vema, bomu hilo la atomiki, lile walilo nalo sasa ambalo litailipua dunia, ninaamini ni kina cha futi mia tatu au nne kwenda chini, na kwa maili mia moja na hamsini mraba. Vema, kama ilikuwa futi elfu kumi chini ya ardhi, moja kwa moja hadi kwenye lava, lingevunja kila mfupa mwilini mwako. Huwezi kuchimbua ulitoroke.

¹⁷⁹ Lakini tunalo kimbilio la bomu, halijatengenezwa kwa feleji, limetengenezwa kwa manyoya, chini ya mbawa Zake, amina, tutainuliwa juu. Hiyo ni kweli. Wakati hilo... Kabla ya hilo bomu kuangushwa, tutakuwa Utukufuni. Kuna nini? Sasa, halafu wanasema sisi ni wazimu. Loo, ikiwa nina wazimu, niache vile nilivyo, ninajisikia vizuri zaidi jinsi hii. Kwa hiyo ninaninii tu... Ninapenda kukaa hivi.

¹⁸⁰ Sasa, angalieni. Sasa, katika wakati wa Sulemani, kila mtu aliamini karama hiyo, loo jamani, kila mtu. Hawakuwa wakizungukazunguka wakisema, “Loo, yeye ni, loo, Assemblies, naye ni, loo, *hili*, na yeye ni, loo, *lile*.” La, wote walikuwa kwa nia moja, waliamini.

¹⁸¹ Na jinsi kila mtu anakuja kwa... kupitia... Hawakuwa na ndege na kadhalika siku hizo, iliwabidi kusafiri kupitia misafara ya ngamia. Nao walipopita, wangesema... kushuka kwenda sehemu zingine za ulimwengu, kasema, “Mnapaswa kusikia kule Palestina, wanaye Mungu kule juu, naye Mungu huyo anajitambulisha Mwenyewe kupitia kwa mwanadamu.”

¹⁸² Sasa, mnaona, ibada ya kikafiri ni kuisujudia sanamu, mungu wa kujibunia, na kuamini kwamba mungu huyo wa kujibunia anazungumza nawe. Ukristo ni kinyume chake, Mungu humchukua mtu aliye hai anayesujudu mbele Zake, na

kunena Maneno Yake Mwenyewe kupitia kwa mtu huyo aliye hai, si kupitia sanamu. Inageuka tu moja kwa moja kutoka kwenye ibada ya kikafiri, ibada ya sanamu, kuelekea kwenye ibada ya Kikristo.

¹⁸³ Sasa, walisema, “Wana mtu huko juu ambaye Mungu wao, wanayemwabudu, huzungumza kupitia mtu huyo kwa upambanuzi.” Loo, ilienea kila mahali mataifa yote yaliwaogopa, wakatuma zawadi na kila kitu. Hakuna vita wakati wa Sulemani. La, alikuwa—alikuwa...walidhani alikuwa mwerevu sana. Haikuwa ni yeye, ilikuwa ni Mungu, Roho Mtakatifu ndani yake ambaye alikuwa akimfanya mwerevu.

¹⁸⁴ Sasa, habari hizo zilishuka duniani kote hadi katika nchi ya Sheba. Na ikiwa utapima kwenye ramani yako, ni mbali sana huko chini, kuvuka Jangwa la Sahara. Naye maskini huyu malkia kafiri, alikuwa kafiri, nao watu wakiingia wakisema, “Loo, mnapaswa kuona kule Palestina, *hivi-na-hivi*, na *hivi-na-hivi*.” Jamani, jinsi wanavyoliwazia hilo!

¹⁸⁵ Sasa, mnajua, imani chanzo chake, ni nini? Kusikia Neno la Mungu. Sasa, maskini mwanamke huyo angesema, “Ati nini?” Mnajua Mungu ndani yake, yeye aliamini kwamba kulikuwa na Mungu, na kwa hiyo wakati imani hiyo ilipoanza kumgusa, ya kwamba kulikuwa na Mmoja, alianza kumtafuta Huyu. Basi kila mtu angeingia, walipoingia katika ufalme wake, misafara ya ngamia ikipita, mnajua, wafanyabiashara, na kadhalika, wakiwa na hariri na kitani, na kadhalika, na mazao, na chochote walichokuwa nacho, wakipita, mbona, angewaita kwenye ikulu yake, aseme, “Je, mlipitia Palestina?”

“Naam.”

“Je, ndivyo ilivyo?”

¹⁸⁶ “Ndivyo ilivyo, ndivyo ilivyo. Wewe kamwe...Watu hao wana moyo mmoja na nia moja. Hujawahi kuona kitu kama hicho maishani mwako. Mungu wao amewapa karama na kuionyesha kupitia mwanadamu, nao wakamfanya mtu huyo kuwa mfalme wao. Loo, jamani. Wote wanaiamini hiyo, kila mmoja wao.”

“Naam, ulipata kuiona?”

“Naam.”

“Je, ni kweli?”

“Hakika, ni kweli.”

¹⁸⁷ Loo, jamani. Anataka kuiona basi, mwajua, unaposikia habari zake. Sasa, aliamua kwamba alikuwa...Akachukua Magombo yote, akaanza kusoma huyo Mungu alikuwa ni nani. Unaona? Alikuwa kafiri, naye akaanza kusoma kile Yehova alichokuwa, kuona asili Yake. Akasema, “Basi hiyo lazima iwe ni asili ya Yehova ambaye anajidhihirisha Mwenyewe ndani ya

mtu huyu, kwa sababu Yehova, wanasema, ni mwenye hekima yote, Naye hutabiri mambo.”

¹⁸⁸ Kwa hivyo sasa, akiwa ni malkia, alikuwa na mengi ya kupitia, ilimbidi aende kwa kasisi wake kafiri na kuomba ruhusa ya kutoka katika kanisa lake. Naam, mnajua nini? Ninawazia yule kasisi kafiri, alisema, unajua, “Lakini unaona, angalia hapa, ewe Msichana, wewe ni malkia, huwezi kwenda kule chini pamoja na kundi hilo lisilo na elimu,” wajua, “huwezi kufanya hivyo, wewe ni malkia. Nao... Unajua nini? Mbona, unajua, ingeninii... ungetoka nje ya tabaka lako ukishuka kwenda kule.”

Naye akasema, “Lakini, bwana, nataka kwenda. Kitu Fulani kinaniambia nataka kwenda.”

¹⁸⁹ “Loo, lakini sisi... huwezi kufanya hivyo, mwanangu, huwezi kufanya hivyo. Sasa, sikiliza, tunajua wanasema kila namna ya mambo haya yote kule juu, ‘Ati walivuka Bahari ya Shamu, nayo ikakauka, na—na wakashushiwa mkate kutoka Mbinguni.’ Lakini, ni hekaya tu, ni bure.”

¹⁹⁰ Mnamsikia maskini ibilisi yuyo huyo akizungumza siku hizi. Ibilisi huchukua mtu wake, lakini sio roho yake. Wala Mungu hamchukui Roho Wake. Anaweza kumchukua mtu Wake, lakini Roho Mtakatifu aliyekuwa juu ya Kristo, alirudi kwa ajili ya Kanisa hata mwisho wa dunia kufanya jambo lile lile.

¹⁹¹ Angalieni. Sasa, maskini wanachuoni hodari na kadhalika wa siku hizo, na maskini lile kundi kubwa mno la Mafarisayo, wangali hai, roho yao iko moja kwa moja juu ya wengine, mnaona, naye Roho wa Mungu angali hai vile vile, akithibitisha Neno Lake, akiendelea. Inategemea kile unachotaka kuamini, hivyo tu.

¹⁹² Sasa, kama tukiangalia... Kisha akasema, “Sasa, hakuna kitu kama hicho.” Kasema, “Sasa, kama kungekuwako na jambo lolote kwake, sanamu zetu, kanisa letu lingekuwa likilifanya.”

¹⁹³ Unapata hilo, jambo lile lile leo hii, “Sasa, kama kuna jambo lolote kwenye uponyaji wa Kiungu, kanisa kuu la *Ninii* lingeliamini, kanisa kuu la *Ninii* lingefanya jambo hilo. Mnaona?” Lakini mnajua, Mungu hufanya mambo ili kujiridhisha Mwenyewe. Hahitaji kumwuliza mtu yeyote kulihusu, Yeye ni Yule ajitoshelezaye Mwenyewe, mnaona, hana haja ya kumwuliza yeyote. Kwa hiyo Mungu alikuwa akifanya hivyo.

Unajua, maskini moyo wako ukianza kuona njaa kwa ajili ya Mungu, hakuna kitu kitakachouzuia. Naye akasema, “Bwana, nitaenda kwa vyovyote vile.”

“Vema, ukienda, nitakupa barua yako ya kanisa.”

¹⁹⁴ Kasema, “Afadhali unipe, kwa sababu niko njiani.” Hivyo yeye... Unaona, hakuna kitakachomzuia mtu anayemjia Kristo

ambaye kweli anamwamini. Unaposikia Neno la Mungu, na kujua linasonga mbele, hakuna kitakachokuzuia, hivyo tu, unakuja kwa vyovyote vile.

¹⁹⁵ Na sasa kumbukeni, maskini mama huyo alikuwa na magumu mengi. Sasa, ninamwona akipakia ngamia zake, na hapa akawazia jambo fulani, akasema, “Sasa, hebu kidogo, kama hiyo kweli ni...kama karama hiyo ni ya kweli, basi nitaiunga mkono.” Kwa hiyo akachukua dhahabu nyingi sana, na ubani, na kadhalika, na kuipakia juu ya ngamia. Akasema, “Nitaenda nayo, lakini ikiwa sivyo ilivyo, basi nitarudisha pesa zangu moja kwa moja.”

¹⁹⁶ Hilo lingeweza kuwafundisha Wapentekoste jambo fulani, kuunga mkono mikutano, na mikutano ambayo—ambayo inachukia kitu kile kile mnachotetea, mnaliacha kanisa lenu lenyewe likose. Wanafanya hivyo Marekani, natumaini ninyi Wakanada hamfanyi hivyo, lakini wanafanya hivyo huko chini kusudi tu wawe maarufu, “Nilichangia *ninii* kwa *hiki-na-hiki*.” Loo jamani, maziwa machunda hayo.

¹⁹⁷ Angalieni. Sasa, huyu hapa. Akakusanya kila kitu, na kuviweka juu ya ngamia zake, pesa hizo zote, dhahabu yenye thamani ya maelfu mara maelfu ya dola. Pia kumbukeni, wana wa Ishmaeli, Waarabu, walikuwa ni wanyang’anyi jangwani wakati huo. Jinsi ingekuwa rahisi kwao, hao wapanda farasi wenda kasi kuingia mbio na kuua kundi hilo dogo la walinzi waliomzunguka malkia huyo, na—na kuchukua fedha hizo, na kurudi mbio katika dakika tano!

¹⁹⁸ Lakini unaona, ikiwa umedhamiria kumjua Mungu, hujui hofu yoyote. Imani haijui hofu. Hiyo ni kweli? Hujali daktari anasema nini, yale mtu mwingine yeyote anayosema, unaamini. Unaona? Naye hakuwa akiwazia juu ya wanyang’anyi, na *hili*, *lile*, na *linginelo*, alikuwa akiwaza kuhusu kufika kule na kumwona Mungu akifanya kazi ndani ya mwanadamu.

¹⁹⁹ Na sasa, kumbuka yeye...Mnadhani ilimchukua mwanamke huyo muda gani? Hakuwa na Kadilaka yenye kiyoyozi ya kusafiria, la, ilimbidi asafiri kwenye mgongo wa ngamia. Mnajua iliuchukua msafara huo wa ngamia muda gani kutoka Sheba hadi Palestina? Miezi mitatu, siku tisini, kupitia jangwa la Sahara lenye joto, mahali penye joto zaidi ulimwenguni, juu ya mgongo wa ngamia, akijaribu kuja kuona karama ya Mungu. Si ajabu Yesu alisema atasimama katika Hukumu na kukihukumu kizazi hiki. Mnaona? Huenda alisafiri usiku, mchana akajilaza katika chemichemi na kusoma yale Magombo, Maandiko, kuona kile Yehova alichokuwa. Hatimaye akafika malangoni.

²⁰⁰ Hakuja, aseme, “Vema,” kama watu wanavyofanya siku hizi, “Nitaingia na kuketi, kama akisema jambo moja ambalo ni kinyume na imani yangu, nitasimama moja kwa moja na kutoka

nje.” Hiyo inaonyesha ujinga. Hiyo ni kweli. Lakini alikuja kukaa mpaka aliposhawishika. Alikuwa amesoma Biblia, aliona kile ambacho Yehova alimaanisha, na kile ambacho Yehova alikuwa, na kile ambacho Yehova alikuwa ameahidi. Alitaka kuona ikiwa huyo Yehova, waliyenena habari Zake, alikuwa ndani ya mtu huyo.

Nami nawazia kasisi wake alimwambia, kasema, “Vema, sasa angalia hapa, huyu hapa Dagoni wetu mkuu, hii hapa sanamu yetu kuu hapa.”

²⁰¹ Akasema, “Naam, nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya wa nyanya yangu aliwahudumia, nao hawajafanya lolote ila kusimama hapo kama sanamu wakati wote. Hawapumui, hawasogei, hakuna kitu kilichotendeka. Nao wanasema Mungu huyu ni Mungu aliye hai, anafanya jambo fulani.” Amina. Ndivyo hivyo. Amina.

²⁰² Ninajisikia kidogo kubarikiwa hivi sasa, naam. Mungu aliye hai, si aliyekufa. Ana faida gani Mungu aliyeweza kufungua Bahari ya Shamu, kama hawezi kufanya vivyo hivyo siku hizi? Mungu ana faida gani ambaye angeweza kumponya mwenye ukoma katika siku zilizopita, kama hawezi kufanya vivyo hivyo leo? Mungu wa kihistoria hafai, kama Yeye si Mungu yeye yule leo. Hiyo ni kweli. Yeye ni Mungu yeye yule leo, jana, leo, na hata milele, Yeye yule, akiomba tu imani ile ile waliyotumia.

²⁰³ Sasa, yeye yuko hekaluni, anafungua mizigo huko nje uani mwa hekalu, anapiga mahema yake, anaweka pesa zake kwenye kona, anaweka matowashi wake karibu wazilinde. Basi kesho yake asubuhi, labda aliamka mapema, yeye na vijakazi wake wadogo waliokuwa pamoja naye, nao wakaingia na kuketi, pengine huko nyuma kabisa kanisani. Nao wakaimba nyimbo zote, nazo baragumu zikapigwa na kila kitu, na baada ya muda kidogo Mchungaji Sulemani akajitokeza.

²⁰⁴ Jinsi watu wote walivyosema, “Loo, Mungu asifiwe, huyo hapo mchungaji wetu.” Nao wakatoka, Mchungaji Sulemani akiwa jukwaani. Naye akatazama siku hiyo, mambo yale yale ambayo alisikia yakisemwa, yakitukia.

²⁰⁵ Na siku baada ya siku akaendelea kusoma yale Magombo. Alingoja hadi kadi yake ya maombi ilipoitwa, ama chochote kile alichokuwa nacho kufika pale, miadi yake na Sulemani. Ndipo alipopanda kwenye . . . hapo mbele ya Sulemani, Biblia ilisema kwamba hapakuwa na jambo lolote lililofichika kwa Sulemani, alifunua kila kitu ambacho alitaka kujua.

²⁰⁶ Je, huyo si ni Mungu yeye yule aliyekuwa ndani ya Kristo, aliyejua siri za moyo? Yeye alisema nini? Aligeuka, sasa, akiwa kafiri, akageuka, naye akasema, “Yote niliyosikia yalikuwa ni ya kweli, na zaidi ya hayo.” Ilikuwa imefanywa kwake, mnaona, alikuwa shahidi wa jambo hilo. Jambo lile lile ambalo Nathanaeli na hao wengine waliona (jana usiku) katika Yesu,

akifanya jambo lilo hilo, akifunua siri za moyo, hapa, miaka elfu mbili na mia tano kabla, hapana, kama miaka mia nane kabla halijatukia, huyu hapa Sulemani alisimama akifanya jambo lile lile ambalo Kristo alifanya alipokuja. Ni Mungu yeye yule. Mnaona?

²⁰⁷ Alisema nini? “Heri walio pamoja nawe wanaoona karama hii ikifanya kazi wakati wote. Heri watu wanaoketi hapa kila siku, na kuona hilo likitendeka wakati wote.” Ndipo akawa mwaminio.

²⁰⁸ Naye Yesu alisema atasimama katika siku za mwisho na atakihukumu kizazi hiki, kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia aone karama ya Mungu ikifanya kazi, akaia mini, nao watu, siku hizi, hawatavuka barabara. Hiyo ni kweli. Hawataendesha gari zuri waende mkutanoni, endapo watafanya chochote, ni kuufanyia mzaha. Naye Kristo mwenyewe alitabiri kwamba kizazi kiovu na cha zinaa ambacho kitakuwa kinatafuta ishara kingepokea ishara ya ufufuo. Si ajabu. Shida ilikuwa nini?

²⁰⁹ Katika kumalizia, nasema hivi, aliona kitu halisi. Hicho ndicho waaminio wa kweli wanachotaka kuona, kitu halisi. Kumbukeni, jambo lile lile linalomwoko mwaminio halisi, humhukumu na kumpeleka kuzimu, asiye mini. Maji yale yale yaliyomwoko Nuhu, yalimzamisha asiye mini. Hukumu ile ile iliyomwoko mwaminio, ilimwua asiye mini. Roho yeye yule, leo hii, ambaye mwaminio humpokea, atamhukumu, katika Siku ya Hukumu, yule asiye mini. Mnaona?

²¹⁰ Hadithi ndogo tu kwa ndugu zangu Wahindi, na wote. Ninapenda kuwinda. Loo, napenda sana kuwinda! Jamani, jamani, hiyo—hiyo ni asili yangu ya pili, uongofu wangu haukuwahi kuniondolea hilo. Nami ni—ningetaka kusimulia hadithi ndogo ya kuwinda hapa, ambapo Mungu aliniambia hasa, mchungaji wenu, Ndugu Byskal, anakumbuka kisa hicho, Ndugu Sothmann, kule nyuma, ambapo Yeye aliniambia yale nitakayofanya hasa, mahali ningeenda, kuro ambaye ningempata, mahali angekuwa amelala, mtu angekuwa amevaa shati la kijani kibichi, na ningemwua dubu mkubwa mkali wa kijivu kabla sijarudi. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli, Ndugu Sothmann? Mamia ya watu niliwaambia.

²¹¹ Nikaenda pale pale, naye Eddie akanisikia nikiisimulia, siku moja kabla hatujaondoka, kule chini. Siku mbili baadaye, alisimama pale pale na kuona kila sehemu yake ikitimia, sawasawa kabisa. Nikawaambia, nikasema, “Hizo pembe zitakuwa na urefu wa inchi arobaini na mbili kamili.”

²¹² Ndipo yule kiongozi akasema, “Ati arobaini na mbili kamili?” Kasema, “Ndugu Branham, baada ya...” Akasema, “Yuko wapi dubu huyo aliye juu ya mlima huu?” Kasema, “Ndugu Branham, kulingana na ulichoniambia, kwamba

utamwua dubu mkubwa wa kijivu kabla ya kurudi mahali aliposimama Eddie Byskal akiwa amevaa shati la kijani kibichi." Naye mke wake alikuwa ameliweka kwenye mkoba wa kambi, naye akaniambia hata hakuwa nalo.

²¹³ Nikasema, "Vema, basi, kutakuwa na mtu ambaye atakuwa nalo, kwa maana litakuwako." Naye alikuwa amevaa shati hilo la kijani kibichi.

Kasema, "Ati kabla hatujarudi huko?"

Nikasema, "Hiyo . . ."

²¹⁴ Akasema, "Ndugu Branham, nilikuwa na ndugu aliyekuwa na kifafa, nawe ukaniambia, akishikwa na kifafa hiki tena, ninyakue shati lake na kulitupa motoni, wala asingekuwa nacho tena." Vema, alifanya hivyo, na Mungu akamponya huo. Sasa, akasema, "Basi siwezi kukosa kuliamini. Lakini dubu huyo atakuwa wapi?"

²¹⁵ Nikasema, "Yeye ni Yehova-yire, Yeye anaweza kujipatia dubu ili kufanya Neno Lake litimie." Ndipo tulipokuwa tu kama nusu maili kutoka kwao, tukiwa kama maili tatu kutoka kwao, tulikuwa karibu nusu maili kutoka kwao. Nilikuwa nimesimama . . .

Akasema, "Ndugu Branham, tuna umbali wa nusu maili tu. Huyu dubu yuko wapi?"

Nikasema, "Usininii . . ." Nikasema, "Ni kitu gani kile, Bud?" Kulikuwa na dubu mkubwa mkali wa kijivu wa futi tisa, mwenye ncha za fedha amesimama juu ya kilima, akinitazama moja kwa moja.

Akasema . . . Tuna yadi mia tano, akasema, "Ndugu Branham, je, uliwahi kumpiga risasi dubu mkubwa mkali?"

Nikasema, "Nimewapiga dubu wengi."

Akasema, "Afadhali umlenge risasi kutoka hapa."

Nikasema, "La, ono lilisema nilikuwa moja kwa moja karibu naye."

Akasema, "Loo, Ndugu Branham!" Akasema, "Mpige risasi mgongoni sasa," kasema, "kwa sababu usipompiga risasi mgongoni, hao ni wapiganaji hatari."

Nikasema, "Najua, lakini huyu katika ono nilimpiga risasi moyoni."

Akasema, "Loo!"

Nami nikasema, "Zidi tu kusonga mbele, Bud."

²¹⁶ Tukaenda kwenye korongo nyingine ndogo, tukapanda, kisha tukawa papo hapo karibu naye, yapata yadi mia mbili, nikasema, "Hii ni sawa kabisa." Nikasema, "Ngoja mpaka aangalie huku." Alionekana kama lundo kubwa la nyasi kavu. Akageuka, akanitazama.

²¹⁷ Nilikuwa na bunduki ndogo, na mara tu alipogeuka na kunitazama nikampiga risasi moja kwa moja kwenye moyo, naye huyu hapa akibingirika kilimani namna hiyo, upesi alivyoweza kuja, namna hiyo. Naye Bud akasimama pale, huku anageuka mweupe kinywani, akasema, “Ndugu Branham, sikumtaka mkononi mwangu.”

Nami nikasema, “Wala mimi sikumtaka.” Hapo . . .

Akasema, “Sasa, kama pembe hizo ni inchi arobaini na mbili hasa nifikapo kule chini, nitashikwa na kifafa cha kupiga mayowe.”

Nikasema, “Afadhali ushikwe nacho papa hapa, kwa sababu ndivyo itakavyokuwa.”

Akasema, “Nina kipimo kwenye begi langu la tandiko.”

²¹⁸ Ndipo tukafika huko chini. Lile ono lilisema m—mkono mdogo ungeshika hizo pembe. Nikasogea karibu na Ndugu Eddie pale, nikasema, “Sasa, mwangalieni mvulana huyo akishikilia hiyo pembe.” Naye akazunguka na kuchukua ule utepe wa kupimia, akautoa, akauweka sehemu ya chini ya kichwa, mkono huo mdogo, mvulana wake, Blaine, aliushika, akaenda pale.

Bud akasema, “Rehema, Ndugu Branham, kamilifu kabisa, inchi arobaini na mbili.”

²¹⁹ Nikasema, “Bud, Yeye hashindwi kamwe, namaanisha, Yeye husema kabisa— . . . sawasawa tu.” Loo, Yeye ni Mungu! Wakati tunapoweza kuona kitu halisi na cha kweli! Hicho ndicho malkia huyo alitaka kuona, kitu halisi.

²²⁰ Nilizoea kuwinda na ndugu yangu nusu-Mhindi, jina lake Bert Call. Yeye ni wa Uingereza, naye anaishi hapa juu, ama, Mwingereza, anaishi huko New Hampshire. Mwindaji hodari, napenda kuwinda pamoja naye, hukuhitaji kujipumbaza kuhusu kumwacha apotee, alijua njia yake ya kurudi. Nasi . . . Lakini alikuwa mtu katili sana niliyewahi kumwona maishani mwangu, mtu huyo alikuwa mwovu sana. Alikuwa na macho kama ya mjesi, na sikuzote alinitazama kwa macho hayo ya mjesi, na kuniogopesha kabisa.

²²¹ Lakini a—alizoea kuniambia . . . Alikuwa akiwapiga risasi watoto wa kulungu, mwajua, watoto wachanga wa kulungu. Sasa, ni sawa, nimeua watoto wa kulungu wakati . . . Ikiwa sheria inasema unaweza kumwua mtoto wa kulungu, umwue, hiyo ni sawa. Ibrahimu alichinja ndama na kumlisha Mungu. Hakuna kitu katika ukubwa wa kitu chochote, au jinsia yake, lakini kuwaua tu kiholela, hiyo ni hatia. Hupaswi kufanya, kuwaua tu kiholela.

²²² Hilo ni jambo moja kuhusu Mhindi, sababu ya kuwa mhifadhi mkuu tuliypata kuwa naye, alichukua tu kile kilichombidi kutumia, kama angeshika wengi

zaidi, aliwaachilia. Mzungu alikuwa mwuaji, walitoka nje, wakawapiga risasi nyati, na kadhalika, kwa ajili ya shabaha. Huyu ndiye mtu mbaya, ni kufanya mambo kama hayo.

²²³ Lakini Bert alikuwa akiwapiga risasi apate tu kujifurahisha, ili kunifanya—kunifanya nijisikie vibaya. Alisema, “Nyie wahubiri ni waoga kama kuku.” Basi hicho ndicho. . . Mnajua kile. . . ? Je, neno hilo linatumika huku juu, *mwoga kama kuku*? “Mwoga kama kuku.” Kasema, “Hiyo—hiyo ndiyo shida yenu nyinyi wahubiri.”

²²⁴ Basi siku moja nilipanda huko juu. Naye alikuwa amejitengenezea filimbi ndogo, kuifanya isikike kama mtoto wa kulungu, na maskini hiyo “brrr” ndogo, wao. . . akilia, kana kwamba alikuwa akimlilia mama yake.

Nami nikasema, “Bert, hutafanya hivyo.”

Akasema, “Loo, wewe mhubiri mwoga kama kuku.” Akasema, “Billy, ungekuwa mwindaji mzuri kama hukuwa mhubiri.”

Lakini ilinibidi kuwawinda wanyama wake yapata kila msimu wa majani kupukutika kwa vyovyote vile, mnaona, kwa hiyo ni—nilimwacha tu aendelee. Kwa hiyo nikasema, “Bert, kweli hutafanya hivyo.”

Akasema, “Kuna ubaya gani kuua mtoto wa kulungu?”

²²⁵ Nikasema, “Hakuna, ila kumpiga tu kumwacha amelala hapo, kwenda na kumpiga mwingine, kutenda tu kikatili,” nikasema, “hilo—hilo ni baya, Bert. Hupaswi kufanya hivyo. Huyu atakua awe dume mkubwa siku moja, labda wa kike, awazae kulungu wengine wengi. Unaweza kuwa na watoto siku moja, waliotaka kuwinda,” na kadhalika.

“La, upuuzi,” akasema, kwa ukaidi kadiri alivyoweza kuwa.

²²⁶ Kwa hivyo siku hiyo ilikuwa imechelewa sana, nasi tuna wale kulungu mikia myeupe huko juu, nawe unanena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kutoroka, yeye ni mwanagenzi kwa mmoja wa hao. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Jamani, atakuwa ametoroka *hivyo*. Ilibidi uwe mwepesi, na kuharakisha, na mwenye shabaha nzuri kumpiga, halafu, baada ya—baada ya kurushiwa risasi mara kadhaa.

²²⁷ Kwa hivyo ilikuwa mwishoni mwa msimu, nasi tulikuwa tumewinda asubuhi yote, hakuna hata mburuzo, yapata inchi sita au nane za theluji. Na kila wakati tunabeba themosi iliyojaa chokoleti yenye moto, ambapo kama tukikumbwa na dhoruba usiku, ama chochote kile, tungeendelea vema, na basi tulikuwa na sandiwichi kwenye koti letu.

²²⁸ Basi yapata saa tano, ndipo nikawazia, “Vema, hata hatujaona mburuzo, wala chochote kile.” Usiku wa mbalamwezi, nao watakula usiku, mnajua, kula, kisha waende mchana, walale chini vichakani, huko nyuma kwenye msitu mnene.

²²⁹ Na kwa hiyo tulikuwa tukifika, karibu kwenye mpaka wa msitu nami nikawazia labda... naye Bert alikuwa akiongoza. Nasi tungepanda juu ya mlima, kisha angejitenga na kwenda njia moja, nami nyingine. Kisha tungekuja, labda tungeingia usiku huo au kesho yake asubuhi, mojawapo, nasi tukimwua kulungu tungejua mahali pa kwenda kumchukua, na kadhalika, kuchukua farasi na kumfuatilia. Kwa hiyo basi, nikawazia, alikuwa...

²³⁰ Akaja kwenye upenyo mdogo kama mara tatu au nne ya ukubwa wa jengo hili hapa, naye kwa namna fulani akachutama juu ya chungu cha theluji, kidogo amechutama. Neno hilo halitumiki hapa, sivyo? Mimi ni mkusini. Kwa maneno mengine, alichuchumaa? Alichuchumaa namna *hii*. Naye a—akashuka pale, ndipo akaenda kutoa kutoka kwenye koti lake. Nilifikiri alikuwa akienda kuchukua sandwichi yake, na kwa hivyo nikaiendea yangu. Nikawazia, “Vema, tutatengana hapa, nitashika njia moja naye nyingine, na kuwinda alasiri ya leo.”

²³¹ Naye akanyoosha mkono akatoa filimbi hii ndogo. Nikasema, “Sasa, Bert!” Naye akanitazama, hayo macho ya mjusi yakinitazama, na kidogo yana dhihaka, kicheko hicho kidogo cha dhihaka usoni mwake, naye akatoa filimbi hiyo ndogo namna *hiyo*, kisha akaipiga, basi alipofanya hivyo, kulungu mkubwa mno akasimama njiani, katikati ya upenyo huo mdogo.

²³² Nikawazia, “Salaala. Loo, amechukua hatua mbaya basi.” Sasa, hilo ni la kigeni, hawatafanya hivyo kwa kawaida, ninyi ndugu Wahindi mnajua jambo hilo, wanapowindwa.

²³³ Ndipo basi, akanitazama, na hayo macho ya mjusi, angecheka, ndipo akaipiga tena, naye huyo kulungu jike akatoka moja kwa moja akaingia kwenye uwazi huo. Sasa, hilo ni la kigeni kabisa kwao, pale, kufanya hivyo.

²³⁴ Sasa, kulungu jike ni mama, mnajua. Ningeweza kuona ninii yake makubwa... Nilikaribia vya kutosha kuona macho yake makubwa, hayo masikio makubwa yamechomoza juu, ni wa kupendeza sana. Alitoka akaja pale pale. Sasa, shida ilikuwa nini? Hakuwa akijifanya, alikuwa ni mama, alizaliwa mama. Silika ya *mama* ilikuwa ndani yake, naye mtoto wake alikuwa analia, hakuogopa chochote, alikuwa anakuja kumtafuta mtoto wake.

²³⁵ Nasi kamwe hatutii risasi kwenye mtutu, kwa hivyo akaingiza risasi, risasi ya punje uyoga ya .30-06, mia moja na themanini... uyoga, akaivuta pale juu, naye alikuwa mlenga shabaha hodari. Basi wakati... Ilikuwa ni Winchester Muundo 70, na alipovuta wenzu chini namna hiyo, mlio wa hiyo bunduki, huyo kulungu akashtuka, akatazama, naye akamwona huyo mwindaji, lakini kamwe hakutimua mbio.

²³⁶ Sasa, mnajua hilo si kawaida. Lakini yeye alikuwa ni mama, mtoto wake mchanga alikuwa taabani, naye alizaliwa mama, naye alikuwa akimsaka mtoto wake mchanga. Basi akamtazama huyo mwindaji, naye, huku ameinua pua yake kubwa juu, akitazama namna *hiyo*, akijaribu kumtafuta mtoto wake mchanga. Yeye... Alikuwa amemsikia akilia, hakuwa anajifanya, alikuwa mkweli. Alikuwa mama.

²³⁷ Nikamwona amemlenga vilivyo, mlenga shabaha hodari sana, nami nikawazia, "Loo, jamani. Ataupiga moyo wake aurusha moja kwa moja upande huo mwingine. Anawezaje kumdanganya hivyo? Anawezaje kuwa katili sana hata kufanya hivyo? Kupiga filimbi hiyo, na kumleta mama kulungu huyo nje hapa kisha kumpiga risasi, nina shaka kama angemchukua."

²³⁸ Nami nikawazia, "Moyo huo mwaminifu wa kulungu huyo utalipuliwa umtoke." Nami nikatazama, nikamwona akimlenga vizuri, nikawazia, "Mara tu mistari hiyo iliyokingama kwenye darubini hiyo itakapoulenga moyo huo mwaminifu, ataulipua kupitia kwake." Nikampa kisogo, nisingeweza kuliangalia.

²³⁹ Nami nikaanza kuomba, nikasema, "Baba wa Mbinguni, anawezaje kufanya hivyo? Anawezaje kufanya hivyo, Bwana? Wala hatanisikiliza nikizungumza juu Yako." Nikasema, "Anawezaje kufanya hivyo?" Nami nilikuwa pale kwa namna fulani nikiomba kwa nafsi yangu nyuma ya kichaka.

²⁴⁰ Nikasikiliza bunduki ifyatuke dakika yoyote, lakini haikufyatuka, nikangojea, haikufyatuka. Nikatazama pande zote, nayo ilikuwa ikienda namna *hii*, asingeweza kuishikilia tena. Akatazama pande zote, machozi makubwa yakitiririka mashavuni mwake, nywele zake nyeusi za Kihindi zikaanguka usoni mwake. Akaitupa hiyo bunduki chini kwenye hilo fungu, akasema, "Billy, nimetosheka. Niongoze kwa huyo Yesu unayezungumzia."

²⁴¹ Ilikuwa ni nini? Aliona kitu halisi. Aliona kitu ambacho hakikuwa ni cha kujifanya, bandia. Aliona onyesho halisi la umama ukimtafuta mtoto wake, kitu ambacho kilikuwa ni halisi. Ee Mungu, tufanye sisi sote kuwa Mkristo wa namna hiyo.

²⁴² Ni wangapi hapa ndani wangependa kuwa Mkristo kadiri huyo kulungu alivyokuwa mama? Moyo wako, hatari, au hakuna chochote kingine, kuona kitu kikubwa, kuona kitu ambacho ni halisi. Basi Mungu, loo, baraka Zake na... .

²⁴³ Na tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja. Kila mmoja wenu kwa moyo wako omba, na kusema, "Mungu, nifanye kuwa Mkristo wa namna hiyo," kimyakimya tu kwa nafsi yako sasa.

²⁴⁴ Ee Mungu, Baba yetu, wajalie watumishi Wako, Ee Baba, msamaha wa dhambi. Utusikie tunapolia, utubariki sasa. Zifunue dhambi zetu miyoni mwetu, na utufanye Wakristo halisi. Jalia neema na rehema zijae miyoni mwetu. Tujalie, Bwana.

²⁴⁵ Waliona kitu halisi, nao walikuwa tayari wakati huo. Waliona kitu ambacho hakingeweza kubuniwa, ilibidi kiwe kitu cha kweli, hakikuwa ni kitu cha kujibunia. Nasi tunaye Mungu, usiku wa leo.

²⁴⁶ Mtu huyo ni shemasi katika kanisa. Pale pale kwenye fungu hilo la theluji, huku mikono yake ikiwa imeikumbatia miguu yangu ya suruali iliyoganda, akasema, “Billy, hapana shaka kuna Mungu mahali fulani.” Kasema, “Je, kuna Mungu anayeweza kunifanya Mkristo, kadiri kulungu huyo alivyo mama?”

Nikasema, “Naam, Bert, Jina Lake ni Yesu. Je, utampokea?”

Akasema, “Kwa moyo wangu wote, Billy, ninampokea.”

²⁴⁷ Nikapiga magoti kwenye theluji, nikatoa hiyo risasi kwenye bunduki yake, nikamkumbatia shingoni mwake kwa mkono wangu, hapo, tukiomba pamoja, alimpokea Yesu kama Mwokozi wake. Hiyo imekuwa kama miaka ishirini iliyopita, yeye ni mshiriki mwaminifu wa Mwili wa Kristo sasa, ndugu wa ajabu.

²⁴⁸ Sasa, huku tunapoomba, ni wangapi hapa, katika uwepo wa Kiungu, mkiwa mmeinamisha vichwa vyenu, wangesema, “Ningependa kuwa Mkristo wa namna hiyo”? Labda hukumkubali Kristo kama Mwokozi wako, nawe ungesema, “Mungu, unirehemu, sikuzote nimetaka kuwa Mkristo, lakini kwa kweli, sijawahi kuona chochote ambacho kingenifanya tu...hakuna kitu halisi kama hicho, lakini ninaamini kweli kwamba kuna Mungu, nami ninataka kumkubali kama Mwokozi wangu.” Je, utainua mkono wako, useme, “Niombe, Ndugu Branham”? Mungu akubariki, bwana. Mwingine? Mungu akubariki, mama. Mwingine? Mungu akubariki, Mungu akubariki, wewe, wewe. Mungu akubariki huko nyuma, mama. Baadhi... Mwingine?

²⁴⁹ Sasa, unaweza kuwa mshiriki wa kanisa, sizungumzi kuhusu ushirika. Ninazungumzia, ni wewe kuwa Mkristo, wa kweli, kifo hakingekuwa na maana yoyote kwako. Unampenda Yesu hata Yeye ni ninii tu...wewe ni...unampenda kama vile mama anavyompenda mtoto wake mchanga. Nawe unajua, unazunguma kuhusu upendo alio nao kwako? Alisema, “Je, mama anaweza kumsahau mtoto wake mchanga anayenyonya?” Kasema, “Anaweza, lakini Mimi siwezi kuwasahau. Majina yenu yameandikwa katika vitanga vya mikono Yangu.”

²⁵⁰ Sasa, malkia wa kusini alikuja kuona hekima ya Sulemani. Huyu hapa Yesu, baada ya mamia haya yote ya miaka, alikuwa akifanya jambo lile lile. Nao... Akasema, “Wao...” Alikuwa kumsikiliza Sulemani. Naye Huyu hapa akiwa na karama ile ile, ila kubwa zaidi, na iliahidiwa ya kwamba, katika siku hii, wangepokea ishara ya ufufuo. Mungu, tufanye halisi. Ombeni sasa. Mungu awe pamoja nanyi. Omba tu, kimya kimya tu peke

yako, ukisema, “Unihurumie, Bwana, sasa ninatubu dhambi zangu zote, ninamwamini.”

²⁵¹ Mungu akubariki, ukiamini kwamba ni . . . imani iko moyoni mwako. Sasa, inueni vichwa vyenu, angalieni huku. Mimi ni ndugu yenu, nimekuja kuwaambia ukweli. Yule Mungu aliyempa Sulemani ile karama ni Mungu yeye yule, usiku wa leo. Yesu alisimama pale, akiwa Mungu ayedhihirishwa katika mwili, na kuwaonyesha hao watu.

²⁵² Sasa, Biblia inatabiri ya kwamba katika siku ya mwisho, Roho wa Mungu atajidhihirisha Mwenyewe kwa njia iyo hiyo, kabla tu ya kuja kwa Mwana wa Mungu, ingekuwa kama ilivyokuwa huko Sodom. Mnaamini hilo? Sasa, hebu Mungu uliyemkubali kama Mwokozi wako binafsi, hebu anene, usiku wa leo.

²⁵³ Ni wangapi wenu enyi watu hapa ambao . . . ? Nitaachana na kadi za maombi wakati uu huu. Ni watu wangapi hapa ambao hawana kadi ya maombi, sasa, huna kadi ya maombi, nawe unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Inua mkono wako, useme, “Nitaamini.” Sawa.

²⁵⁴ Sasa, angalieni huku, kwa muda kidogo tu. Nikiwa mgeni kwenu . . . Sasa, kama Yesu angesimama hapa, usiku wa leo, amevaa suti ii hii aliyonipa, miaka kadhaa iliyopita, sasa, kama ukimjia, nawe ukasema, “Bwana, utaniponya?” Asingeweza kufanya hivyo, tayari ameshalifanya. Mnaamini hilo, sivyo? “Kwa kupigwa Kwake . . .”

²⁵⁵ Lakini angeweza kukuthibitishia ya kwamba Yeye alikuwa ni Kristo. Na njia pekee ungejua hivyo, si kwa jinsi alivyokuwa amevaa, si makovu juu Yake, lakini huduma ambayo angekuwa nayo, Yeye angekuwa ni Neno. Nayo Biblia ilisema, “Neno la Mungu lina makali kuliko upanga ukatao kwili, na Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli, semeni, “Amina.”

²⁵⁶ Sasa, Biblia ilisema kwamba Yesu, sasa, ni Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu. Hiyo ni kweli? Sasa, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, vipi kuhusu imani yako kumgusa, kisha uangalie na kuona . . . ? Sasa, ikiwa mimi . . .

²⁵⁷ Sikilizeni. Je, mnaamini angekuwa na uhusiano wowote na mnafiki? Yesu? La, bwana. Unaamini angejijhusisha Mwenyewe na uongo? Si Mungu wetu. La. Lakini Mungu wetu anawajibika kwa Neno Lake. Je, hiyo ni kweli? Na kwa unyenyekevu, anaruhusu haya yafanyike, si kwa sababu inamlazimu, bali kuwaonyesha watu ya kwamba Yeye ni Mungu na anatimiza ahadi Yake, Mungu.

²⁵⁸ Baadhi yenu ninyi watu huko nyuma, ninyi Waanglo-Sakson, mnaamini hilo kwa moyo wenu wote? Inua mkono

wako, useme, “Ninaamini, kabla sijaona jambo lolote likifanyika kweli, ninaamini.”

Enyi Wahindi, mnaamini kwa moyo wenu wote? Inua mkono wako.

²⁵⁹ Sasa, sasa, tena, nitakuomba, wewe usiye na kadi ya maombi, inua mkono wako. Sasa, huna kadi ya maombi, inua mkono wako, wazungu huko nyuma. Vema.

²⁶⁰ Sasa, ninawatakeni muombe. Ninyi watu huko nyuma, ombeni na kusema, “Bwana Yesu, mhubiri huyo hanifahamu, lakini Wewe unanifahamu.” Sasa, unaweza kushusha mkono wako chini na kuomba, na kusema, “Bwana Yesu, ikiwa Wewe ni Kuhani Mkuu, nijalie nikuguse, halafu ugeuke,” kama yule mwanamke aliyegusa vazi Lake, Naye akageuka na kusema, “Ni nani aliyenigusa Mimi?”

Ndipo Paulo, au, Petro akasema, “Bwana,” akamkemea, “wote wanakugusa Wewe.”

Akasema, “Lakini naona nimekuwa dhaifu.” Nguvu, uweza ulimtoka.

²⁶¹ Sasa, kama maskini mwanamke mmoja akimgusa, akitumia karama ya Mungu, kama maskini mwanamke mmoja akimgusa ilimfanya kuwa dhaifu, vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi, niliyeokolewa kwa neema? Lakini Yeye alisema nini? “Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya, nyingi kuliko hizi mtazifanya. . .” Sasa, la King James linasema, “kubwa zaidi.” Lakini. . .katika tafsiri ya asili. . .Hakuna chochote kingeweza kuwa kubwa zaidi, aliwaponya wagonjwa, akawafufua wafu, akayakomesha maumbile, akafanya kila kitu. Lakini “nyingi kuliko hizi mtazifanya,” kote ulimwenguni, mnaona, “kwa maana naenda kwa Baba.”

²⁶² Sasa, wewe omba. Unajua shida yako, basi omba. Na hebu. . .Kama hujawahi kuona jambo lolote halisi likifanywa, Naye ataonekana hapa, usiku wa leo, katika Uwepo Wake. . . Sasa, si mimi na ninii zangu. . .Haidhuru nina karama kiasi gani, huna budi kuwa na imani pia, maana imani yako ndiyo inayoiendesha, si mimi.

²⁶³ Yule mwanamke, aligusa vazi Lake Naye akawa dhaifu, hiyo ilikuwa ni mwanamke akitumia karama ya Mungu. Lakini alipoondoka nyumbani kwa Lazaro, akaenda zake, akawa. . . kisha akarudi, na akamfufua mtu aliyekuwa amekufa siku nne, Yeye kamwe hakusema alikuwa dhaifu wakati huo, hiyo ilikuwa ni Mungu akitumia karama Yake. Mnaamini hilo? Maana alisema kaburini, mnajua, “Na—nakushukuru, Baba, tayari umenisikia, kwa—kwa ajili ya hawa nilisema hilo.” Mnaona? Akasema, “Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe.” Hiyo ndiyo sababu Yeye hakurudi walipoagizia aje. Sasa, omberni.

264 Na kama mimi ni mtumishi wa Mungu. . . Sasa, kama mtu yeyote anadhani hili ni la uongo, njoo hapa ukalifanye, hebu tukuone ukilifanya, endapo ni la uwongo. Kimya kabisa. Basi sivyo, ni la Mungu. Ni Biblia ya Mungu. Sasa, ninyi aminini. Na muamini tu sasa, nyote. . .

265 Nina wasiwasi. . . Hii ni mikutano kumi na moja mfululizo kwangu, nami nimechoka kabisa. Mnajua hilo. Usiku baada ya usiku, kila usiku, nguvu, uweza, na mchana kutwa, Yeye atanituma huko chini pembeni na kusema, “Simama hapa, kutakuwa na jamaa mmoja atakayekuja kwenye kiti cha magurudumu.” Hayo ni maono makubwa, haya ni madogo, ninyi mnayasababisha haya. Hayo ni yale ambayo Mungu hutoa, kasema, “Mtu huyu anakuja, na alifanya jambo *fulani* wakati *fulani*. Atakuwa anajisukumiza pembeni, sema naye tu, na kumwinua kutoka kwenye kiti cha magurudumu, kisha uende zako. Mtu yeyote asijue ni nani anayefanya hivyo.” Mnayasikia hapa magazetini, na mambo kama hayo. Hakuna anayejua ni nani. Ananituma huko chini, kasema, “Fanya hivi.” Mnaona? Huyu ni Mungu akitumia karama Yake. Mnaona?

266 Sasa, wewe fanya hivyo. Tumia karama ya Mungu na kusema, “Ewe Kuhani Mkuu wa Mungu, jalia nikuguse Wewe. Nawe umtumie Ndugu Branham kunena nami, na kama utaniambia tu shida yangu ni ipi, na kile. . . hili, ama jambo fulani ambalo, moyoni mwangu, ninaliombea, nitaamini kwa moyo wangu wote.” Ndipo basi utaweza, tuseme, kama yule mama kulungu, kama. . . Utaona kitu halisi, kama alivyoona Bert Call.

267 Sasa, hapa. Hapa, Hii hapa. Asante, Bwana. Angalieni *huku*. Ni wangapi wameiona ile picha gazetini, usiku wa leo? Mmeiona? Je, aliionyesha hapa? Vema. Mnajua ile Nguzo ya Moto mliyoiona gazetini? Hiyo hapo. Imesimama papo *hapo*. Iko juu ya maskini mwanamke mmoja, anayeketi huko nyuma kabisa, kuelekea kule nyuma, maskini mama mmoja. Amevaa miwani, kidogo ni mwembamba, anasumbuliwa na mizio.

268 Je, unaamini, Dada? Ulinua mkono wako dakika chache zilizopita, hukuwa na kadi ya maombi. Huna. . . huna kadi ya maombi, sivyo? Simama kwa miguu yako. Hiyo ndiyo shida yako? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Na kama mimi ni mgeni kwako, pungu mkono wako *hivi*. Nataka kukuuliza jambo fulani. Hivi sasa ulihisi hisia tamu kweli, sivyo? Halisi tu. . . Ninaiangalia ile Nguzo ya Moto moja kwa moja, ikimzunguka mwanamke huyo moja kwa moja, sasa hivi. Imani yako imekuponya. Yesu Kristo, unaona.

Sasa, mnaamini?



ALIYE MKUU KULIKO SULEMANI YUPO HAPA SWA62-0725

(A Greater Than Solomon Is Here)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumatano jioni, tarehe 25 Julai, 1962, kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Legion huko Port Alberni, British Columbia, Canada, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2023 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org